**Atupwa** jela miaka 20 kwa kuhifadhi wahamiaji haramu

UKURASA 3



**Waziri** ageuka mbogo huduma mbovu za ardhi

UKURASA 4




UKURASA 11


# Nipashe

Jumamosi Februari 27, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580504

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# JPM awabana mawaziri malipo mafao wastaafu

• **Akataa** kulipa bil. 19/- zilizokopwa CRDB, aagiza TAKUKURU ichunguze... *Endelea ukurasa 2*



Rais Dk. John Magufuli akikagua majengo ya madarasa ya Chuo cha Taaluma cha Polisi Kurasini, baada ya kuyafungua mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO


**UKURASA WA 4**

**MADUKA DAWA YAFUNGIWA KWA KUTIBU WAGONJWA**

HALMASHAURI ya Ushetu mkoani Shinyanga imeyafungia maduka mawili ya dawa za...

**UKURASA WA 4**

**TANESCO YAKAMILISHA UMEME TRENI YA KISASA**

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) limekamilisha ujenzi wa vituo vinne vya kusafirisha...

**UKURASA WA 8**

**ASISITIZA UTALII NDANI KUONGEZA PATO LA TAIFA**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, amesisitiza kuwa fursa zilizoko kwenye...


## Watendaji waonywa usajili wa VICOBA

UKURASA 3

## DC ashtukia nyaraka feki za vigogo kumiliki ardhi

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


**MICHEZO** **KIM ATAJA UMUHIMU WA YONDANI STARS** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na waumini wa Kiislam baada ya kumalizika kwa Sala ya Ijumaa, katika Masjid Raudha Daraja Bovu Wilaya ya Magharibi "A" Unguja, jana. **PICHA: IKULU**

# JPM awabana mawaziri mafao wastaafu

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli amewataka mawaziri kushughulikia mafao ya watumishi wa umma, ili kusiwe na ucheleweshaji wa stahiki zao hizo wanapostaafu.

Kiongozi huyo wa nchi alitoa agizo hilo jana wakati wa hafla ya kuweka jiwe la msingi kwenye kiwanda cha ushonaji Bohari Kuu ya Jeshi la Polisi na kufungua majengo ya Chuo cha Taaluma ya Polisi, Kurasini, Dar es Salaam.

Rais Magufuli aliyasema hayo baada ya awali, Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Simon Sirro, kubainisha kuwapo maofisa wa polisi wastaafu ambao hawajapewa mafao yao kwa muda mrefu.

"Kuna suala limezungumzwa hapa la wastaafu wa Jeshi la Polisi kutolipwa mafao yao, ila msemakweli ni mpenzi wa Mungu, ninawashangaa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, nina uhakika hata raia hapa wanawashangaa.

"Mstaafu wako amefanya kazi yake nzuri katika miaka yake yote amemaliza Jeshi la Polisi bila tatizo lolote, anatakiwa kulipwa mafao yake ambayo yapo.

"Waziri utakaa ofisini kusubiri bila ya kwenda kuwaombea, kwa nini? Katibu Mkuu utakuwa umekaa ofisini tu? Naibu Katibu Mkuu utakuwa umekaa ofisini tu? Rais Magufuli alihoji.

Rais Magufuli alihoji sababu za viongozi hao kutochukua majina yao na kwenda nayo Wizara ya Fedha na Mipango na kuitaka wizara hiyo ilipe fedha zao.

"Tatizo mawaziri wangu hawawasiliani. Kwa hiyo, mnaendeleza watu wa chini kupata shida. Huu ni wajibu wa Wizara ya Mambo ya Ndani, nikificha nitakuwa mnafiki na mimi sitaki kuwa mnafiki.

"Nikiwa Waziri wa Ujenzi, tulipopata shida za makandarasi, nilikuwa ninakwenda kufanya fujo pale Wizara ya Ujenzi. George Simbachawene (Waziri wa Mambo ya Ndani, inawezekana ulikuta hizo habari. Wala hawakunipenda Wizara ya Ujenzi. Ninaenda Wizara ya Fedha ninataka fedha za makandarasi na walikuwa wanalipwa.

"Kwa hiyo, IGP ukistaafu, Simbachawene (Waziri) hatashughulikia malipo yako. Hilo ndiyo ujue. Hili ni tatizo la wakubwa wenu wizarani, sitaki kusema kwa unafiki, ninasema hapa wanisikie," alisema.

Rais Magufuli alisema haiwezekani wastaafu wa polisi wamsubiri Rais akashughulike nao.

"Mbona jeshini hawanisubiri? Niwaombe wastaafu kama mpo hapa, mumlaumu Simbachawene na naibu wake, katibu mkuu wake, naibu katibu mkuu wake na wakurugenzi ili mumuunganishe na IGP kwa sababu hawapigi kelele huko, huo ndiyo ukweli! Wakitaka wastaafu kulipwa watalipwa, haiwezi kuchukua hata siku tano," alisema.

Rais Magufuli alibainisha kushangazwa na kitendo hicho akihoji kulikoni maofisa wenye nyota na wamefanya kazi kubwa na kukoswa kupigwa risasi na majambazi, wamestaafu bila kulipwa mafao yao.

"Hii siyo sawa! Hii ni changamoto kwa viongozi wakubwa wa wizara wala msiniambie. Mlitakiwa mniambie kwamba Waziri wa Fedha au Katibu Mkuu Wizara ya Fedha amekataa kutoa fedha, ili nimlazimishe kutoa fedha kwa nguvu. Wanaowacheleweshea haki zenu ni hawa wakubwa wanaokaa kwenye viyoyozi," alisema.

# DC ashtukia nyaraka feki za vigogo kumiliki ardhi

**Na Godfrey Mushi,** HAI

WATU 17 wanaotuhumiwa kutengeneza nyaraka feki za umiliki wa ardhi iliyotengwa kwa ajili ya matumizi ya serikali ikiwa na ukubwa wa ekari 22.4, wamenaswa katika mikono ya Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya.

Jana, Ole Sabaya alisema eneo hilo ambalo awali lilikuwa limetengwa kwa shughuli za dampo, lilikuwa limeshaingizwa kwenye mpango kabambe wa mipango miji wa wilaya hiyo mwaka 1988.

Kwa mujibu wa Ole Sabaya, watu hao wanadaiwa kumilikishwa eneo hilo kwa ukubwa tofauti tofauti na Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Sanya Station (wakati huo), Sabore Mollel, sasa Kijiji cha Jiweni kilichopo Kata ya Muungano, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Hai.

Ole Sabaya alisema mwaka 1994, wakati wanauziana eneo ambalo serikali ya Kijiji cha Sanya Station ilikuwa haina mamlaka ya kuuza, mtendaji huyo wa kijiji alikuwa anagawa maeneo kwa kadri alivyotaka.

"Sasa TAKUKURU (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa) ninakuomba, kabla ya leo (jana) jua kuzama, mtu anaitwa Sabore, mtafute popote kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi mkamateni na nitawapa nyaraka zote za namna Sabore alivyozitengeneza.

"Mkurugenzi (Yohana Sintoo) kuanzia sasa eneo liko chini yako, mmenielewa. Nimeona watu wachache sana kama watano, ambao ukifuatilia historia yao, ndiyo ambao hawana aidha mikono ambayo ina rushwa na ulaghai kati ya miongoni mwa hawa.

"Nitakupa majina yao uyajumuishe kwa kuwapa kiwanja kimoja kimoja au viwili, waendelee na maisha yao. Hao wengine wote waondoke na wasisogelee eneo hili," aliagiza.

Ole Sabaya alionya wananchi wa eneo hilo akisisitiza: "Nimesema wasisogelee kwenye eneo hili kama hawataandikiwa barua na mkurugenzi. Saimon Sairungui, Tajiri Mameki, Kembe, Lazaro Shuwaka, mnaojiita wamiliki mko wapi? Mmetengeneza nyaraka feki 17 na hampo, mnajua mlichokifanya."

Akionyesha kukerwa na hujuma hiyo, Ole Sabaya alimwambia Ofisa Ardhi wa Wilaya hiyo, Straton Thobias, kwamba alitamani kutoa uamuzi huo, alipaswa awaambie hao wananchi kwamba mwaka 1984, eneo hilo lilishakuwa limeingizwa kwenye mipango miji.

Alisisitiza kuwa kwa kawaida eneo kama hilo likishaingizwa kwenye mpango kabambe, maana yake linatengua hati zote za kimila.

Akiwa katika eneo hilo, Ole Sabaya alibainisha nia yake ya kutaka kulitwaa eneo lingine la ekari 11 lililoko jirani na eneo hilo katika muda usiozidi siku saba kuanzia sasa, ambalo amemilikishwa mfanyabiashara mkubwa wa mjini Moshi.

# ... Aagiza uchunguzi mkopo wa mabilioni

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuchunguza mkopo wa Sh. bilioni 19 uliokopwa na Manispaa ya Temeke katika Benki ya CRDB kwa ajili ya kulipa fidia wananchi.

Alitoa agizo hilo jana katika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi kwenye kiwanda cha ushonaji Bohari Kuu ya Jeshi la Polisi na kufungua majengo ya Chuo cha Taaluma ya Polisi Kurasini, Dar es Salaam.

Ni maagizo aliyoyatoa baada ya awali, Mbunge wa Temeke, Dorothy Kilave, kumwomba serikali iisaidie manispaa hiyo kulipa deni la Sh. bilioni 12.195 kati ya Sh. bilioni 19 zilizokopwa CRDB kutekeleza mpango wa DNDP uliowezesha kulipa fidia kwa wananchi na kujenga zahanati na barabara.

Katika majibu yake, Rais Magufuli alisema: "Unajua mambo ya ajabu sana, Manispaa mmekaa, mkakwenda kuzungumza na CRDB, mazungumzo yale wala hayajulikani mlikuwa mnazungumza nini, yawezekana mazungumzo yale yalikuwa ya kificho, labda palikuwa na asilimia, mmeshindwa kulipa, mnataka serikali ilipe hilo deni.

"Kwa hiyo, tuna manispaa ngapi? Halmashauri ngapi zikawa zinafanya mikopo yao ya ovyo ovyo ya wizi, serikali ije kulipa? Hiyo msahau, mtalibeba wenyewe.

"Kwanza, ni kukosa nidhamu ya fedha za serikali kwenda kuzihusisha katika mikopo kwenye commercial bank (benki ya biashara). Halafu mnakwenda kulipia fidia. Kwa vyovyote, hiyo fidia waliotoa maeneo, lazima walizungumza na watendaji wa halmashauri.

"Ndiyo wizi ulivyokuwa unafanyika. Mbunge ninajua haukuwapo (ni mbunge mpya), lakini ngoja nikutandike kwa sababu wamekutuma kuzungumza -- hakuna fedha itakayotolewa na serikali.

"Sana sana serikali inaweza kutuma wakaguzi kuchunguza hizo fedha zilikuwa na ulazima wa aina gani. Kamanda wa TAKUKURU ninaomba ufuatilie hili wamenisaidia kulieleza hapa," aliagiza.

Alisema anataka kujua fedha hizo ni nani alikwenda kufanya mazungumzo na benki hiyo na wamilikiwa wa maeneo waliofidiwa.

"Je, fedha zilizolipwa zilistahili? Je, majengo yaliyojengwa yana thamani ya Sh. bilioni 12? Unaweza ukakopa Sh. bilioni 12, ukalipa fidia halafu ukajenga majengo ya Sh. milioni 500?

"Hapa ninauona ufisadi mkubwa unaelea tu. Ninajua watakulaumu waliosema lakini umefanya vizuri kujichongea hapa. Hakuna hata senti tano itakayotolewa, mtandikwe hayo madeni, shauri yenu," alisisitiza.

Rais Magufuli alisema wakienda kwa utaratibu wa namna hiyo hawatafika na kueleza hayo yalikuwa mazoea ya baadhi ya halmashauri, kupanga mambo kumbe wanatengeneza asilimia za mgao wa fedha katika maeneo yao.

"Kwa sababu mmeharibu hili, hata lile eneo la TBA (Wakala wa Majengo) silitoi kwenu, litabaki kuwa la TBA, nao wana uwezo wa kufanya biashara," alisema.

Awali, Mbunge Kilave alimweleza Rais Magufuli kuwa miaka ya nyuma, walikopa Sh. bilioni 19 CRDB kwa ajili ya kulipa fidia wananchi waliokuwa wanawabomolea nyumba zao ili kupisha miradi ya maendeleo.

# Watendaji waonywa usajili VICOBA

**Na Salome Kitomari,** MTWARA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imetangaza mwisho wa usajili wa vikundi vya jamii, maarufu kama VICOBA, huku ikionya watendaji kuhusu kukwamisha kazi hiyo.

Imesisitiza kuwa mwisho wa usajili huo ni Aprili 30, mwaka huu, na kusisitiza kwamba baada ya muda huo kumalizika, havitaruhusiwa kufanya shughuli zao huku ikiwataka maofisa maendeleo ya jamii wasigeuke kuwa kero kwa wananchi wanaotaka kusajili vikundi vyao, ikiwamo kuhakikisha mfumo unafanyakazi muda wote.

Akizungumza wakati wa kufunga mafunzo ya wiki moja kwa maofisa maendeleo ya jamii wa mikoa ya Mtwara na Pwani, Ofisa Maendeleo ya Jamii kutoka TAMISEMI, Zahara Msangi, alisema ikifika tarehe hiyo, hakuna kikundi kitaruhusiwa kuendelea na shughuli zake. Akifunga mafunzo hayo, Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Dustan Kyobya, aliwataka maofisa hao kuharakisha usajili na kuwafikia wananchi walioko kuliko kusababisha kero ya wote kwenda halmashauri.

"Nawaagiza wakurugenzi wa halmashauri kusimamia usajili wa vikundi hivi ili kuhakikisha kila kikundi kimesajiliwa. Utaratibu huu unakwenda kuvitambua vikundi vya huduma ndogo za fedha kuanzia kubadili majina kutoka kuitwa VIKOBA. Kusajili kikundi hakutabadili mwenendo wa uendeshaji wa kikundi lengo la sasa ni kutambua vikundi," alisema.

Kwa mujibu wa mkuu huyo wa wilaya, utaratibu wa pili wa kusimamia vikundi utakuja jinsi ya kukopesha, kwa jinsi mfumo ulivyoundwa na kutengeneza lengo ni kutambua katika jamii kuna vikundi vingapi.

Kyobya alisema Halmashauri ya Nanyamba ina kata 17, vijiji 87, vitongoji 323, mitaa 9, Mtwara DC kata 110, vitongoji 433, Manispaa kata 18 na mita 111 na kwamba ni lazima kuvifikia vikundi vyote na kuvisajili ndani ya siku 30 zilizobaki.

"Wilaya ya Mtwara kama ya kwanza maofisa wake kupewa mafunzo ya mfumo ni muhimu wawe wa kwanza kukamilisha usajili wa vikundi, washirikishe watendaji wa mitaa, vijiji na vitongoji kwa kuwa VICOBA vipo ngazi ya chini kabisa.

"Tunataka mfumo ufanye kazi vizuri na wawafuate wananchi na wawasajili kuondoa usumbufu, wananchi wajue viambatanisho vyote muhimu wanavyotakiwa kuwa navyo, hakikisheni usajili hauwi kero kwa wananchi, bali usajili ufanyike katika utaratibu ambao utasaidia wanachama wa vikundi husika," alisema.

Pia alisema utaratibu wa kukopeshana utabaki vile vile, lengo ni kupata taarifa za jumla za wananchi walio kwenye vikundi hivyo, ikiwamo majina ya wanakikundi, idadi ya vikundi na walikokopa lengo ni fedha za vikundi visipotee.

"Baadaye utakuja mfumo mwingine wa wakopaji na amekopa wapi na wapi na wakipotea ni rahisi kufutwa na kuepusha mikopo chechefu au kuumiza kwa wanachama wanaokopa na kutoroka," alisema.

Naye Meneja wa Huduma Ndogo za Fedha na Maduka ya Kubadilisha Fedha, Victor Tarimu, alisema kuna madaraja manne yaliyotambuliwa kisheria na kila moja lina kanuni zake na mamlaka iliyokasimiwa kusimamia.

Alisema daraja la kwanza ni benki zinazotoa huduma ndogo za fedha ambazo zinasimamiwa na BoT. La pili ni taasisi zinazotoa mikopo bila kupokea amana za umma ikijumuisha kampuni za kukopesha, watoa huduma ndogo kwa njia za kudijitali na watu binafsi wanaokopesha.

Aidha, alisema hadi sasa wamepokea maombi 663, leseni 293 zimeshatolewa na mengine yamkatalia na baadhi yako katika hatua za usajili hadi Februari 2, mwaka huu.

# Jela miaka 20 kuhifadhi wahamiaji haramu

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

MAHAKAMA ya Wilaya ya Bagamoyo, imemhukumu Julius Shija, Mkazi wa Makurunge wilayani hapa miaka 20 jela au kulipa faini ya Sh. milioni 20 baada ya kukutwa na hatia ya kuwahifadhi wahamiaji haramu 16 nyumbani kwake.

Wakati mkazi huyo akipewa adhabu hiyo, mahakama hiyo imewahukumu raia 83 wa kigeni kwenda jela miaka miwili kwa makosa ya kiungia nchini kinyume cha sheria.

Mwingine aliyehukumiwa ni Eliah Lekule, mkazi wa Arusha miaka mitatu jela baada ya kukutwa na hatia ya kuwasindikiza wahamiaji haramu wawili katika stendi ya mabasi ya Bagamoyo kwenda Dar es Salaam.

Katika hukumu iliyotolewa mahakamani hapo na Hakimu Mkazi Mwanakombo Mmanya, raia wa Ethiopia 81, Somalia mmoja na Malawi mmoja wamehukumiwa kwenda jela miaka miwili au kulipa faini Sh. 500,000 kila mmoja.

Awali, mwendesha mashitaka wa Idara ya Uhamiaji Mkoa wa Pwani, Fadhili Festo, alidai mahakamani hapo kuwa wahamiaji haramu hao walikamatwa Januari na Februari, mwaka huu, katika maeneo tofauti ya Wilaya ya Bagamoyo.

Kutokana na hukumu hiyo, Mkuu wa Uhamiaji Mkoa wa Pwani, Paul Eranga, aliwaonya wamiliki wa mabasi wanaotumika kuwasafirisha wahamiaji haramu.

Eranga alisema kwa sasa wahamiaji haramu wanaopita katika mkoa huo na wamebadilisha njia ambazo walikua wakitumia awali za kupanda boti na bodaboda badala yake wanasafirishwa kwa mabasi ya abiria.

Alisema basi lolote litakalokamatwa likiwa limebeba wahamiaji haramu baada ya kesi kumalizika litataifishwa na kuwa mali ya serikali.

Eranga pia aliwaonya raia wa Tanzania ambao wamekuwa na tabia ya kuwahifadhi na kuwasaidia wahamiaji haramu kuvuka hapa nchini, kuacha mara moja biashara hiyo kwa kuwa kwa atakayekutwa na hatia, hatua za kisheria zitachukiwa kama onyo kwa wengine.

Alisema pamoja na Rais John Magufuli kutoa msamaha kwa wahamiaji haramu, raia wa Ethiopia na Somalia kurudi kwao, bado wameendelea kukamatwa kwa kuvunja sheria za nchi na za kimataifa zinazomtaka raia wa nchi nyingine kuingia akiwa na kibali halali.

Eranga alisisitiza kuwa idara yake katika mkoa itaendelea kupambana na wahamiaji haramu hadi suala hilo litakapokoma.


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya Gadau Auctionmart & Company Ltd, Mopeh Company Limited na Mase International Ltd Kwa idhini tuliyopewa Finca Microfinance Bank Ltd tunatoa muda wa siku 14 kwa wadaiwa walioorodheshwa kwenye jedwali hapo chini wawe wamelipa madeni wanayodaiwa na Finca microfinance bank ltd, Kinyume na hapo tutalazimika kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mali walizoweka kama dhamana ya mkopo. Tarehe za kufanya minada zitatolewa kwa njia ya vipeperushi na magari ya matangazo kwenye sehemu dhamana zilipo.

| Na. | Kampuni inayohusika | Jina La mdaiwa | Dhamana Inayouza Na Mahali Ilipo |
|---|---|---|---|
| 1 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Gerald E Temba | Stoo Ya Bidhaa, Gari-Fuso Mitsubishi T564 Adw, |
| 2 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Ramadhani A Sanze | Nyumba Ipo Kiegea 'A' Manispaa Ya Morogoro Pamoja Na Stoo Ya Bidhaa. |
| 3 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Vedasto J. Kilendu | Kiwanja Chenye Nyumba Vipo Kisanga Pamoja Na Stoo Ya Bidhaa |
| 4 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Abdalla Baraza Kitega | Kiwanja Kipo Mikumi Mjini Wilaya Ya Kilosa, Vifaa Vya Nyumbani Na |
| 5 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Suleimani S. Saidi | Kiwanja Na Nyumba Vipo Kiegea Manispaa Ya Morogoro |
| 6 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Niwaeli Ismail Mrutu | Kiwanja Kipo Kihonda Manispaa Ya Morogoro |
| 7 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Solomon Agustino Nkuja | Kiwanja Pamoja Na Nyumba Vipo Kiegea 'A' Pamoja Na Stoo Ya Bidhaa |
| 8 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Yahaya Issa Msungi | Kiwanja Kipo Kwamchambe Pamoja Na Stoo Ya Bidhaa |
| 9 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Malaki L. Kinyamagoha | Stoo Ya Bidhaa, Kiwanja Kipo Mkundi Na Kingorwila Manispaa Ya Morogoo Na |
| 10 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Peter M. Mdoho | Kiwanja Kipo Mkundi, Pamoja Na Stoo Ya Bidhaa |
| 11 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Abdul Rahm Abdalla | Kiwanja Kipo Kisore, Vifaa Vya Biashara Na Stoo Ya Bidhaa |
| 12 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Daniel B Gabriel | Nyumba Ipo Dakawa, Morogoro Na Stoo Ya Bidhaa |
| 13 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Shakilly Gaudensi Rock | Nyumba Iko Dakawa, Morogoro Na Stoo Ya Bidhaa Na Vifaa Vya Biashara |
| 14 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Hamisi A. Mkali | Nyumba Ipo Mlimani- Mkundi Norogoro Na Stoo Ya Bidhaa |
| 15 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Sylivanus Maro Bartazary | Kiwanja Kipo Makunganya Na Foundation Morogoro Pamoja Na Stoo Ya Bidhaa Na Vifaa Vya Biashara |
| 16 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Remmy Juma Komanya | Kiwanja Kipo Kiegea Kwa Mkude Morogoro, Stoo Ya Bidhaa Na Vifaa Vya Biashara |
| 17 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Dickson L. Matemelela | Nyumba Ipo Kipera- Mlali/Mzumbe Morogoro, Na Vifaa Vya Biashara Vipo Kiwanja Cha Ndege Karibu Na Kituo Cha Polisi |
| 18 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Amani E Mmassy | Kiwanja Kipo Kingolwira Manispaa Ya Morogoro, Stoo Ya Bidhaa Na Vifaa Vya Biashara |
| 19 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Simon J. Mzee | Nyumba Ipo Kiegea 'A' , Stoo Ya Bidhaa Na Vifaa Vya Biashara |
| 20 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Abdallah M. Mohamed | Nyumba Ipo Dakawa Manispaa Ya Morogoro |
| 21 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Bianka Peter Minishi | Kiwanja Kipo Kinyerezi Mafisa, Kwa Mwarabu, Stoo Ya Bidhaa Na Vifaa Vya Biashara |
| 22 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Pricusy A Bitanteye | Kiwanja Kipo Kiegea-Mkundi Morogoro, Stoo Ya Bidhaa, Vifaa Vya Biashara |
| 23 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Evodi U Assenga | Kiwanja Na Nyumba Vipo Lukobe Juu Morogoro Na Stoo Ya Bidhaa |
| 24 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Shukuru M Kagoma | Nyumba Ipo Dakawa Morogoro, Na Stoo Ya Bidhaa |
| 25 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Mohamed Hemed Kolela | Nyumba Yenye Kitalu No.215 Block 'Ss 'Kipo Mkuzo, No.1649 Block 'Ss' Kipo Mkuzo Plot 265 Block'bbb' Kipo Mkuzo Na Kiwanja Na Nyumba Kipo Lizaboni. Songea Mjini |
| 26 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Anna A Komba | Kiwanja Na Nyumbavipo Lizaboni ,Kiwanja Kipo Ruhuwiko Na Motor Vehicle –Toyota Allion Yenye Namba Ya Usajili T-775 Dqc |
| 27 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Johnson John Mapunda | Mali Za Nyumbani Na Machine Za Kusagia |
| 28 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Bonifasi Fabian Mluga | Kiwanja Chenye Nyumba Vipo Ruhuwiko Kanisani- Manispaa Ya Songea |
| 29 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Ally Alfredi Mlalila | Kiwanja Chenye Nyumba Vipo Mshangao Na Gari- Nissaan Caravan Namba T859 Ipo Songea |
| 30 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Zaidifu M Mtalisi | Mali Za Nyumbani, Mali Zisizohamishika Na Inventory Vipo Songea Mjini |
| 31 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Jovin Caspary Ngonyani | Mali Za Nyumbani, Mali Zisizohamishika Na Inventory Vipo Songea Mjini |
| 32 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Juni Filipo Namwanja | Mali Za Nyumbani, Mali Zisizohamishika Na Inventory Vipo Songea Mjini |
| 33 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Hemed S Sain | Kiwanja Chenye Nyumba Vipo Zyagwila Chipaka Tunduma Na Gari- Mitsubishi Canter Namba T 194 Bag |
| 34 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Ebelino Bernad Mwalongo | Kiwanja Chenye Nyumba Vipo Ilindi- Ilemi-Mbeya Na, Kiwanja Chenye Nyumba Yenye Kitalu Namba 2057,Block C Vipo Mtaa Wa Mtongani Kunduchi. |
| 35 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Zuena J Mwanyanje | Kiwanja Chenye Nyumba Vipo Ndola Mbalizi Mbeya Na Kiwanja Chenye Nyumba Vipo Nkuyu – Nsalala Mbeya |
| 36 | Gadau Auction Mart & Company Limited | Richard L Simba | Kiwanja Chenye Nyumba Vipo Melelan Tunduma Na Kiwanja Chenye Nyumba Vipo Majengo Mapya Tunduma |
| 37 | Gadau Auction Mart & Company | Abdul Lufunyo Kidugogo | Kiwanja Chenye Nyumba Vipo Mtaa Wa Sokoni-Igawilo Mbeya City |
| 38 | Mase International ltd | Betina Mussa Ulaya | Nyumba- Kishiri "B"-Mwanza |
| 39 | Mase International ltd | Eva Tondi Mafwele | Nyumba-Nyamhongolo-Mwanza |
| 40 | Mase International ltd | Rymos Samson Munis | Nyumba-Ihayabuyaga-Geita |
| 41 | Mase International ltd | Andrea Nchinika Majanga | Boma_Ugweto-Shinyanga |
| 42 | Mase International ltd | Sabina Gadiga | Kiwanja-Bulengahasi-Katoro |
| 43 | Mase International ltd | Aman M.Gastor | Kiwanja-Kigoto-Buhongwa -Mwanza |
| 44 | Mase International ltd | Kalimu Msigwa Magadula | Nyumba-Mwatulole-Geita |
| 45 | Mase International ltd | Yusuph Majaliwa Almas | Nyumba-Buhongwa-Mwanza |
| 46 | Mase International ltd | Ortmary G.Komba | Kiwanja-Bombambili-Geita |
| 47 | Mase International ltd | Martin C.Lunguya | Nyumbani-Nyabusozi-Biharamulo |
| 48 | Mase International ltd | Rashana Bonifance Byemerwa | Buswelu-Mwanza |
| 49 | Mase International ltd | Cosmas A.Abdalah | Nyumba -Nyankumbu-Geita |
| 50 | Mase International ltd | Heriet W.Masaki | Kiwanja -Igoma-Mbugani |
| 51 | Mase International ltd | Amos J.Mwambepo | Nyumba(boma)-Kakebe-Mwanza<br>Kiwanja-Magaka-Mwanza |
| 52 | Mopeh company limited | Sara G. Fitwangile | Nyumba iliyopo Nyahanga Kahama |
| 53 | Mopeh company limited | Paulina D. Chundu | Nyumba iliyopo Nyahanga Kahama |
| 54 | Mopeh company limited | Maryceana M. Mwahu | Kiwanja lilichopo Nyahanga Kahama |
| 55 | | Hemed S. Rashid | Kiwanja kilichopo Mbulu Kahama |
| 56 | Mopeh company limited | Christopher M. Manengo | Nyumba iliyopo kiwanja na.1176 Bukkokmbe Kahama |
| 57 | Mopeh company limited | Thomas E. Shayo | Nyumba iliyopo kiwanja na. 88 kitaluESokkola Kahama |
| 58 | Mopeh company | Stephano E. Batano | Nyumba iliyopo Igomelo Kahama |
| 59 | Mopeh company limited | Maige C. Makanza | Nyumba iliyopo MLUNGA Kahama |
| 60 | Mopeh company limited | Emanuel S. Mashingi | Kiwanja kilichopo Kahama |
| 61 | Mopeh company limited | Stella R. Gwiyago | Nyumba iliyopo Iyanga Kahama |
| 62 | Mopeh company limited | Salehe M. Mogena | Kiwanja kilichopo Mbulu Kahama |
| 63 | Mopeh company limited | Ally S. Ally | Kiwanja kilichopo Mhongolo Kahama |
| 64 | Mopeh company limited | Michael B. Mtabazi | Nyumba iliyopo Kahama |
| 65 | Mopeh company limited | Emanueli Clement Messu | Nyumba iliyopo Kahama |
| 67 | Mopeh company limited | Mathayo C. Madebwa | Nyumba iliyopo Kahama |
| 68 | Mopeh company limited | Andrerw James | Kiwanja kilichopo Kahama |
| 69 | Mopeh company limited | Mathew Nkuye7 | Kiwanja kilichopo Kahama |
| 70 | Mopeh company limited | Hobokela J. Mwakarindile | Kiwanja kilichopo Kahama |
| 71 | Mopeh company limited | Aloyce F. Mbwana | Kiwanja kilichopo Kahama |
| 71 | Mopeh company limited | Salum Hussein Kagussa | Kiwanja kilichopo Kahama |
| 72 | Mopeh company limited | Rajabu M. Robert | Kiwanja kilichopo Kahama |
| 73 | Mopeh company limited | Celestine L Magembe | Kiwanja kilichopo Kahama |
| 74 | Mopeh company limited | Robert M Gumali | Nyumba iliyopo Mbulu Kahama |
| 75 | Mopeh company limited | Mbaruku R. Mroto | Nyumba iliyopo Shunu Kahama |
| 76 | Mopeh company limited | Tumpe N. Mwaitamwa | Kiwanja kilichopo Isaka Kahama |
| 77 | Mopeh company limited | Rukia N. Mohamed | Nyumba iliyoko Isaka Kahama |
| 78 | Mopeh company limited | Elizabeth P. Mwenda | Kiwanja kilichopo Ushirombo Kahama |
| 79 | Mopeh company limited | Sophia S. Mugusu | Nyumba iliyopo Mbulu Kahama |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi Wa Dhamana Ni Kwa Kuwasiliana Na Dalali.
2. Mnunuzi Atalipa Asilimia 25% Ya Bei Iliyofika Siku Ya Mnada Na Salio La Asilimia 75% Atalipa Ndani Ya Siku Kumi Na Nne Tokea Siku Ya Mnada, Na Endapo Mnunuzi Atashindwa Kumalizia Salio La Asilimia 75% Ndani Ya Siku Kumi Na Nne Basi Mnunuzi Atakuwa Amepoteza Haki Zake Zote Na Pesa Alizolipa Awali Hata Rudishiwa Na Dhamana Itauzwa Upya.
3. Gharama Za Kubadili Umiliki Ni Za Mnunuzi, Kumbuka Vigezo Na Masharti Kuzingatiwa.
4. Gharama Za Kumtoa Mdaiwa (Mwenye Nyumba Au Wapangaji) Ni Za Mnunuzi.

**Wote Mnakaribishwa**

**Kwa Maelezo Zaidi Wasiliana Na:**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Gadau Auction Mart And Company Ltd**
**S.L.P 40855, Dar Es Saalam,**
**Simu; 0714 635599/ 0785 636864**

**Mkueugenzi Mtendaji,**
**Mopeh Company Ltd**
**Dar Es Salaa, P. O. Box 590,**
**Mob.,+255 (0))785 335544,(0)713 639979,+255 (0,+255(0)755 731072**
**E-Mail:Mopehltd20@Gmail.Com -**
**Dar Es Salaam – Tanzania**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Mase International Mwanza**
**Simu: 0784717164**

## Maduka dawa yafungiwa kwa kutibu wagonjwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Ushetu mkoani Shinyanga imeyafungia maduka mawili ya dawa za binadamu kwa kosa la kutoa huduma za kitabibu ikiwamo kuchoma sindano, kusafisha vidonda na kuwaongezea maji wagonjwa.

Hatua hiyo ni kinyume cha masharti ya maduka hayo ambayo yalisajiliwa kama maduka ya kuuza dawa.

Halmashauri hiyo pia imedhibiti uuzwaji holela wa dawa za binadamu zinazoibwa katika vituo vya serikali za kifua kikuu (TB) na kwenda kuuzwa katika maduka ya dawa, zahanati na vituo vya afya vinavyomilikiwa na watu binafsi.

Mfamasia wa Halmashauri hiyo, Alphonce Malunde, aliyabainisha hayo jana wakati wa kikao maalum kati ya watoa huduma wa maduka binafsi 40, kilichokuwa na lengo kuwakumbusha umuhimu wa kuzingatia maadili ya kazi na vibali vyao katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Alisema katika ukaguzi uliofanyika wiki iliyopita, walibaini kuwapo kwa baadhi ya maduka kutoa huduma kinyume na usajili wao hali ambayo inaweza kuhatarisha usalama wa afya za wananchi hususani katika maeneo ya vijijini kwa kuchoma sindano na kuwaongezea maji wagonjwa.

"Badala ya kuuza dawa kulingana na usajili wenu, mnaanza kuwahudumia wagonjwa kwa kuwachoma sindano, kusafisha vidonda na kuwawekea dripu za maji kinyume cha maadili ya usajili wa vibali vyenu vinavyotolewa na baraza la famasia nchini," alisema Malunde.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Ushetu, Dk. Nicodemus Senguo alisema kuna baadhi ya maeneo wamiliki wa maduka wamekuwa siyo waaminifu wanaamua kuuza dawa ambazo zinakaribia kwisha muda wake.

Alisema wanaendelea kuchukua hatua kali za kisheria kwa watakaobainika kufanya hujuma za dawa na kwamba haiwezekani Halmashauri ya Ushetu iwe maficho ya uuzaji wa dawa zilizokwisha muda wake na kuhatarisha afya za wananchi.

Mkurugenzi Halmashauri hiyo, Michael Matomora, alisema kuna baadhi ya wamiliki wa maduka ya dawa wanashirikiana na watumishi wa umma kuhujumu vituo vya afya vya serikali kwa kuiba dawa za kifua kikuu(TB) na kuwauzia kwa bei ya chini zaidi.

Aliongeza kuwa wamebaini baadhi ya wamiliki wa zahanati kufanya upasuaji mdogo kwa wagonjwa wanaofika kutibiwa kinyume na utaratibu wa usajili wa vibali vyao.

Mwenyekiti wa wamiliki wa maduka, zahanati na vituo vya afya binafsi katika halmashauri hiyo, Mary Lema, alikiri baadhi yao kwenda kinyume cha usajili.



Wamiliki wa maduka binafsi ya dawa za binadamu 40 katika Halmashauri ya Ushetu, mkoani Shinyanga, wakila kiapo cha maadili ya kuzingatia miongozo ya serikali kuhusu uendeshaji wa biashara ya dawa za binadamu, mbele ya Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Michael Matomora (hayupo pichani), jana. **PICHA: SHABANI NJIA**

# Waziri awa mbogo huduma mbovu ardhi

**Na Munir Shemweta,** NJOMBE

WAKATI Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ikifanya jitihada mbalimbali kuhakikisha sekta ya ardhi inapiga hatua katika kupanga, kupima na kumilikisha ardhi, Mkoa wa Njombe kupitia halmashauri zake umeonekana kuwa nyuma.

Hatua hiyo imemfanya Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk Angeline Mabula, kueleza kutoridhishwa na utoaji huduma za sekta ya ardhi mkoani hapa.

Dk. Mabula alisema hayo juzi wakati wa kikao cha kazi baina yake na watendaji wa sekta ya ardhi na wakurugenzi wa halmashauri za Mkoa kilichofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Mji wa Njombe.

Akisoma taarifa ya utekelezaji kazi za ofisi ya ardhi mkoa, Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Njombe, Christopher Mwamasage, alisema tangu kuanzishwa ofisi ya ardhi Machi, mwaka jana, ofisi imetekeleza majukumu mbalimbali ikiwamo kuandaa michoro 59 ya mipango miji.

Hata hivyo, katika taarifa yake, halmashauri za Makete na Ludewa zimeonyesha kutofanya vizuri kwa kushindwa kuidhinisha hata mchoro mmoja.

Pia halmashauri hizo na ile ya Njombe, zimeshindwa kufanya lolote katika urasimishaji makazi huku katika utekelezaji kazi za upimaji na ramani mkoa ukiwa umeidhinisha mashamba matatu pekee na halmashauri ya Wilaya ya Njombe ikiidhinisha ramani na kiwanja kimoja.

Katika utoaji hati na makusanyo ya kodi ya pango la ardhi, Mwamasage alisema hati 1,136 zilitiwa saini na mkoa ulikusanya Sh. 774,346,269 kati ya Bilioni 5.3 ulizopangiwa kukusanya mwaka wa fedha 2020/21.

Sambamba na hilo, alisema mkoa ukipeleka wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi 22 katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya wanaodaiwa Sh. 294,930,957. Kutokana na maelezo hayo, Naibu Waziri alionyesha kutoridhishwa na huduma za sekta ya ardhi zinazotolewa na kuzijia juu halmashauri Makete na Ludewa kwa kuwa nyuma sana katika kutekeleza majukumu yao.

"Hakuna eneo linalohitaji urasimishaji, umilikishaji hata wa mashamba hata hati za kimila. Hii inasikitisha sana na kwa staili hii hatuwezi kufika, yaani Makete sifuri hakuna chochote. Kwa hali hii mnawasaidiaje wananchi?" alihoji. Kwa mujibu wa Naibu Waziri, kwa mwenendo ulioonyeshwa na halmashauri za Makete na Ludewa haina maana ya kuwa na ofisi za ardhi za mkoa na kusisitiza kuwa baadhi ya wakurugenzi wa halmashauri wanaona hali hiyo ni sawa wakati wao ni mamlaka za upangaji katika maeneo yao.

Aliwataka watendaji wa sekta ya ardhi kubadilika na kufanya kazi kwa weledi na kujitahidi kufanya vizuri katika utendaji kazi ambapo aliwaeleza kuwa kila mkuu wa idara ya ardhi au ofisa ardhi mteule atapimwa kutokana na utendaji wake ikiwamo kiasi cha fedha alizokusanya katika kodi ya pango la ardhi.

# TANESCO yakamilisha umeme treni ya kisasa

**Na Joseph Mwendapole,** MOROGORO

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) limekamilisha ujenzi wa vituo vinne vya kusafirisha na kupoza umeme utakaotumika kwa ajili ya treni ya kisasa (SGR) kwa asilimia 99 na kazi iliyobaki ni kuunganisha nishati hiyo tu.

Hayo yalisemwa jana mjini hapa na Meneja Msimamizi wa Ujenzi wa Mradi wa Umeme wa SGR kutoka Kinyerezi hadi Kingoruwila mkoani hapa, Mhandisi Albano Sembua.

Alikuwa akizungumza na wahariri waandamizi na waandishi kutoka vyombo mbalimbali vya habari nchini waliotembelea kuona maendeleo ya ujenzi wa mradi huo.

Alisema ujenzi wa mradi huo una urefu wa kilometa 159 kuanzia Kinyerezi, Dar es Salaam hadi Kingorwila mkoani Morogoro ukiwa na nguzo 462 na zote zimeshajengwa pamoja na kuvuta nyaya.

Aliwaambia wahariri hao kuwa mradi ulianza Januari, 2019 na umekamilika mwaka jana.

"Mradi huu umegawanyika sehemu kuu mbili, kwanza kujenga miundombinu ya kusafirisha umeme kutoka Kinyerezi hadi hapa Kingorwila na kazi ya pili ni kupanua kituo cha umeme cha Kinyerezi kazi zote mbili zimekamilika.

"Ujenzi umefikia asilimia 99 na unafadhiliwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100 na fedha zilizotumika ni Sh bilioni 71.1 na mpaka sasa hivi na tumeshafanya malipo kwa mkandarasi Sh. bilioni 60 ambazo ni sawa na asilimia 84," alisema Mhandisi Sembua.

Pia alisema kinachosubiriwa kwa sasa ni kuunganisha umeme huo katika vituo vinne vya umeme wa SGR ambavyo vimejengwa Pugu, Ruvu, Kidugalo na Kingorwila.

"Kazi ya kuunganisha umeme itaanza wiki ijayo na umeme ambao utazalishwa kwa ajili ya SGR ni wa uhakika na hautakatika hata siku moja kwani vyanzo vyake ni vya uhakika na maalum kwa ajili ya mradi huu tu na kuna laini ya umeme inayotoka Kinyerezi na kuna laini ya umeme ya Morogoro kuja SGR," alisema

"Kwa hiyo ikitokea laini ya Kinyerezi imeleta hitilafu basi laini ya Morogoro itatumika, pia tunayo laini nyingine ya umeme wa Ubungo ambayo nayo imepita Kinyerezi kuja hapa kwa hiyo tunaweza kutumia umeme wa Ubungo,"alifafanua.

Kuhusu faida za mradi huo wa SGR, alisema TANESCO wamepata mteja mkubwa ambaye ni Shirika la Reli Tanzania (TRC) ambaye atahitaji umeme kwa ajili ya treni hiyo ya kisasa inayotumia umeme.

Kuhusu uwezo wa umeme unaozalishwa kwa ajili ya SGR, Mhandisi Sembua alisema laini hiyo inauwezo wa kubeba umeme wa megawati 500 lakini mahitaji ya sasa ya TRC ni megawati 70.

Aliongeza kuwa vituo vinne ambavyo wamevijenga kazi yake kubwa ni kupunguza umeme unatoka Kinyerezi ambao unakuwa kilovoti 220, hivyo lazima upungue hadi kilovoti 27.5 ambao ndio unaingizwa kwenye mfumo wa SGR.

"Mradi huu ni maalum kwa ajili ya reli ya kisasa na tangu Kinyerezi hadi Kinguruwila na hawajaunganishia mteja mwingine zaidi ya TRC peke yake kwa ajili ya reli tu,"alisema na kuongeza

"Sababu ya kuzalisha megawati 500 kwa ajili ya SGR, tunaamini huko mbele ya safari TRC wanaweza kuamua kuongeza miundombinu kwa ajili ya treni ya kisasa, hivyo tumeamua kuwawekea mapema," alisema

# RITA yawanoa wasajili vizazi

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, ameagiza watendaji wote wanaohusika na usajili wa vizazi na vifo kuweka mikakati itakayowezesha wananchi katika maeneno yao kusajiliwa ili kuwaondolea usumbufu wa kutokuwa na nyaraka wanapohitaji huduma nyingine.

Alitoa rai hiyo juzi jijini Mwanza katika hotuba yake iliyosomwa na Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Dk. Philis Nyimbi, wakati wa kufungua mafunzo kwa makatibu tawala wa wilaya na maofisa tarafa wa mkoa huo yaliyoandaliwa na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) yatakayosaidia kutekeleza majukumu yao ya usajili wa vizazi, vifo, ndoa na talaka kikamilifu.

Alisema umuhimu wa nyaraka mbalimbali zinazotolewa na RITA unaendelea kuongezeka, hivyo lazima kuwe na mkakati wa kuwaelimisha wananchi kujisajili na kuwe na mikakati mahsusi itakayowezesha wananchi wengi zaidi kupata huduma kwa wakati.

Mongella aliwapongeza RITA kwa hatua ambazo wanaendelea kuchukua katika kuboresha mfumo wa usajili kupitia Mkakati wa Kitaifa wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu ambao unaendelea kutekelezwa kupitia programu mbalimbali.

Aliongeza kwamba Mpango wa Usajili wa Watoto wa Umri Chini ya Miaka Mitano umeleta matokeo chanya kwa kuwawezesha watoto kupata cheti cha kuzaliwa karibu na maeneo wanayoishi ambapo na takwimu zake zimepatikana na kutumika katika kupanga mipango ya maendeleo.

Mongella aliwapongeza RITA kwa kuandaa mafunzo hayo, akisema huenda baadhi ya watendaji katika ofisi za wilaya ni wageni katika nafasi hizo, hivyo mafunzo yataongeza ufanisi.

Aliwataka washiriki kuzingatia mafunzo wanayopata na kuwataka kutunza miongozo wanayopewa ili iwasaidie watendaji wengine siku za usoni.

Akizungumzia huduma za mirathi na wosia, Mongella aliwaonya wananchi, hasa ndugu na jamaa wa karibu wa marehemu ambao wamekuwa na tabia za unyanyasaji na uporaji wa mali za marehemu baada ya mazishi. "Ninawasihi viongozi wenzangu tutoe elimu kwa wananchi wetu kuanzia sasa wajenge utamaduni wa kuandika wosia mapema na waondokane na dhana mbaya kwamba ni uchuro.

"Dhana hii siyo sahihi kama kufa tutakufa tu na kuacha matatizo makubwa ya ndugu kugombania mali," alisema Mongella.

Kaimu Mkurugenzi wa Msaada wa Haki za Kisheria wa RITA, Lina Msanga, alisema sheria imetamka wazi kwamba kila tukio la kizazi, kifo, ndoa na talaka linapotokea, lazima lisajiliwe na kuhifadhiwa katika daftari la Msajili Mkuu wa matukio hayo ambaye ni Kabidhi Wasii Mkuu.

"Usajili ni takwa la kisheria, lakini kuna sehemu kama watumishi wa umma hatutekelezi ipasavyo majukumu yetu na ndiyo maana leo hii tupo hapa kuwapatia mafunzo maalum kuhusu sheria na miongozo mbalimbali itakayowasaidia kutekeleza majukumu yenu," alisema.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Chama cha Mabalozi wa Usalama Barabarani Tanzania (RSA-Tanzania), Augustus Fungo (kushoto), akikabidhi tisheti maalumu ya chama hicho kwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Ronald Makona, wakati wa zoezi la utoaji wa elimu ya masuala ya usalama barabarani kwa wanafunzi wa shule mbalimbali, ili kuzuia ajali za barabarani mkoani humo jana. Kulia na Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani wa mkoa huo, Zauda Mohammed. **PICHA: JAMES LANKA**

# Ufaransa yazitaka nchi tajiri kutoa chanjo bure

**Na Salome Kitomari**

RAIS wa Ufaransa, Emmanuel Macron, amesema asilimia tano ya chanjo zake za homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya Corona, zitasambazwa barani Afrika na kuzitaka nchi zingine tajiri kufanya hivyo.

Hiyo ni kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana, jijini Dar es Salaam na Balozi wa Ufaransa nchini, Frederic Clavier.

"Kukabiliana na corona ni jambo zito kwa sekta ya afya ambalo linaweza kupata suluhisho kwa mbinu mbalimbali. Nchi zenye uchumi mkubwa ni lazima zionyeshe ushirikiano kwa nchi za uchumi wa chini na kati kwa kuwahakikishia upatikanaji na usambazaji wa haraka wa chanjo hizo," alisema Rais huyo. Alisema katika mkutano wa G7 wa Baraza la Ulaya, Rais Macron alizishawishi nchi za Ulaya, Marekani na nchi tajiri duniani kutoa asilimia tatu hadi tano ya chanjo zake kwa nchi za Afrika ili kukabiliana na ugonjwa huo ambao ni tishio.

"Utaratibu huu uhusishe kwa kuchangia chanjo kwa kuwauzia kwa bei ndogo au kutoa kama msaada kwa nchi za kipato cha chini na cha kati," alisema.

Katika mahojiano yake na gazeti la Financial Times Februari 17, mwaka huu, Rais Macron aligusia umuhimu wa dunia kuhakikisha usambazaji wa chanjo hizo duniani.

"Sisi si kisiwa, watu wetu zaidi ya milioni 10 wana familia maeneo mbalimbali duniani. Katika dunia ya utandawazi, chanjo isiwe ya ubaguzi, tutapoteza wote iwapo nchi za uchumi wa chini zitaachwa nyuma kwenye chanjo," alisisitiza.

Aidha, vipaumbele katika kuharakisha usambazaji wa chanjo, wadau wa kimataifa wameunganisha nguvu zao na kuchangia Mabilioni ya Dola za Marekani kwa COVAX ambayo ni programu maalum ya Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) katika kupambana na corona.

Pia kikao cha G7 kilifanyika kimtandao Februari 19, mwaka huu, ikiwa ni mara ya kwanza tangu Aprili, mwaka jana na mchango uliongezeka kufikia Sh. bilioni 7.5.

Rais Macron alibainisha mambo ya kipaumbele kuhakikisha chanjo inafika Afrika kwa haraka, huku akisema si gharama na kwamba wakitangaza mabilioni ya fedha na usambazaji wa chanjo unaweza kufanyika kwa miezi sita, tutapoteza kuaminiwa na rafiki zetu wa Afrika, haitasaidia kupambana na kusambaa kwa maambukizi ya corona.

Alizitaka jumuiya ya kimataifa kuisaidia Afrika kupata chanjo kuliko kuwafikiria watu wake pekee, huku akisema wafanyakazi wa afya katika mji wa Dakar nchini Somalia anahitaji chanjo kwa haraka.

"Ndiyo maana Ufaranza imekuja na jitihada za G7 kuitaka Ulaya na Marekani kusambaza dozi milioni 13 hasa kwa wafanyakazi wa afya milioni 6.5 walioko Afrika. Kila nchi tajiri inakaribishwa kuelekeza asilimia 3 hadi 5 ya chanjo zake," alisisitiza.

Pia alitaka chanjo hizo kuuzwa kwa bei nafuu huku akitaka kuwajengea uwezo Afrika kutengeneza chanjo zao, uwazi na utaratibu wa gharama za chanjo ili nchi hizo zimudu gharama, pamoja na kusaidia taasisi za Afrika kuwa na zana za kupambana na corona.

Balozi wa Ufaransa nchini, aliahidi kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Wazee katika wito uliotolewa na Rais Macron.


GADAU AUCTION MART & COMPANY LIMITED
Head Office: P.O.BOX 40855 Dar es Salaam - Pugu station Bangulo
Mob: + 255 714 635599/ + 255 785 636864/ + 255 756 753 584
Branch: Mkombozi Bank Agrey Street - Kariakoo/ Mwanza Rufiji Street
Branch: Kilombero Rusha Morogoro
Email: gadauauctionmart@gmail.com/gadauauctionmart@yahoo.com
hashimugadau@yahoo.com

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA NA NOTICE YA SIKU KUMI NA NNE (14) ZA KULIPA DENI LOTE.

Kwa idhini tuliyopewa na BANK YA NBC tutauza kwa mnada wa hadhara DHAMANA MBALIMBALI ZA WADAIWA WA BANK HIYO. Mnada utafanyika kuanzia tarehe 13/3/2021 HADI Ukomo mahali zilipo dhamana kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni.

UFUATAO NI MCHANGANUO WA MAJINA YA WADAIWA, DHAMANA NA MAHALI ZILIPO:

| S/N | ACCOUNT NAME | COLLATERAL OWNER | PLOT NO./PLOT LOCATION | BRANCH | DATE OF AUCTION |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | HAMZA JUMA KISINGILE | HAMZA JUMA KISINGILE | CT NO.1784-MBYLR, L.O. NO.127776, PLOT NO. 54, BLOCK 'D', MAKAMBAKO URBAN AREA I.N.O HAMZA KISINGILE. | MAKAMBAKO | 13/03/2021 |
| 2 | HAMZA JUMA KISINGILE | HAMZA JUMA KISINGILE | CT NO.5667-DLR, L.O. NO.95247, PLOT NO.70 BLOCK 'D' MAKAMBAKO URBAN AREA I.N.O HAMZA JUMA KISINGILE. | MAKAMBAKO | 13/03/2021 |
| 3 | BONIPHACE SELELI | BONIFACE GODFREY SELELI | CT NO. 36509, LO NO. 372261, PLOT NO. 19 BLOCK 'PP' IPULI AREA,TABORA MUNICIPALITY I.N.O BONIFACE GODFREY SELELI | TABORA | 13/03/2021 |
| 4 | JACKSON O NYANJE | OMARY MARIAM NYANJE | CT NO.13355-MBYLR, L.O. NO.295648 PLOT NO.1 TUNDUMA URBAN AREA I.N.O. OMARY MARIAM NYANJE. | TUNDUMA | 20/03/2021 |
| 5 | JULIUS MASIAGA NTAGERA | MATOGORO MASIAGA | CT NO.31622-LRMWANZA, L.O. NO.366714,PLOT NO.28,HIGH DENSITY, BLOCK 'F', NYAMWAGA ROAD AREA, TARIME TOWNSHIP AUTHORITY I.N.O MATOGORO MASIAGA | TARIME | 21/03/2021 |
| 6 | SIMON CHARLES NGAGANI | SIMON CHARLES NGAGANI | CT NO.28092-LR MWANZA, L.O. NO.194846, PLOT NO.213 BLOCK SOMANDA (MD) BARIADI URBAN AREA I.N.O. SIMON CHARLES NGAGANI. | SHINYANGA | 17/03/2021 |
| 7 | | FANUEL ELISHA KIFUNYU | CT NO.16959-LR MWANZA, L.O. NO. 181306, PLOT NO. 867 BLOCK 'O' EXTENSION MAJENGO KIGOMA / UJIJI MUNICIPALITY.I.N.O. FANUEL ELISHA KIFUNYU | SHINYANGA | 15/03/2021 |
| 8 | VEDASTUS KALELA | VEDASTO JOHN NTAMITORIZO | CT NO. 23023-LR MWANZA, LO. NO. 388463, PLOT NO. 141, BLOCK 'F', HIGH DENSITY, MAJENGO KAHAMA URBAN AREA I.N.O. VEDASTO JOHN NTAMITORIZO | KAHAMA | 20/03/2021 |
| 9 | | VEDASTO JOHN NTAMITORIZO | CT NO.23026-LR MWANZA, L.O. NO. 388462, PLOT NO. 554, BLOCK 'O', LOW DENSITY, NYASUBI KAHAMA URBAN AREA I.N.O. VEDASTO JOHN NTAMITORIZO. | KAHAMA | 20/03/2021 |

**MASHARTI YA MNADA**
1. Dhamana zitauzwa "kama zilivyo " as where is basis"
2. Mnunuzi atakayeshinda atalipa malipo ya awali ya 25% ya bei ya mnada siku ya mnada na 75% katika muda wa siku 14
3. Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la 75% katika muda uliopangwa hapo juu hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hatimiliki, kutwaa nyumba/dhamana kumtoa mmiliki wa awali (ikiwa bado hajatoka hadi wakati wa mnada) na gharama nyinginezo zitakuwa juu ya mnunuzi.
5. Wateja wote mnakaribishwa kuonana kukagua nyumba muda wote isipokuwa usiku.

**WOTE MNAKARIBISHWA**
**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:**
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**GADAU AUCTION MART AND COMPANY L.T.D**
**S.L.P 40855, DAR ES SAALAM, SIMU; 0714 635599/ 0785 636864**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Namungo zikipania fainali Afrika inawezekana

**WAWAKILISHI** wa Tanzania kwenye michuano mikubwa na inayoongoza kwa utajiri barani Afrika kwa ngazi ya klabu, Simba na Namungo wameonyesha cheche na kwa kuwashtua wapinzani wao katika mashindano Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika msimu huu.

Simba ambayo inaiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa, tayari imeshinda mechi zake mbili za hatua ya makundi, hivyo kuongoza Kundi A mbele ya Al Ahly ya Misri na AS Vita ya DR Congo zenye pointi tatu kila moja huku Al-Merrikh ya Sudan ikiburuza mkia baada ya kupoteza mechi zake mbili za mwanzo.

Aidha, Simba imeonyesha inaweza kufika mbali kwani mbali na kumfunga bingwa mtetezi wa michuano hiyo, Al Ahly kwa bao 1-0 zilipokutana hapa nchini, pia iliibuka na ushindi kama huo ikiwa ugenini DR Congo dhidi ya AS Vita katika mechi yake ya kwanza.

Kadhalika, Simba ndiyo timu pekee katika michuano hiyo kushinda mechi zote mbili za mwanzo, lakini ikiwa miongoni mwa timu nane ambazo hazijaruhusu nyavu zake kutingishwa katika hatua ya makundi msimu huu.

Ushindi huo na rekodi hiyo huku ikiwa moja ya timu iliyoonyesha kiwango cha juu hadi sasa, ni wazi kama wachezaji, benchi la ufundi na uongozi wa klabu hiyo wataendelea kuwa kitu kimoja na malengo yao yakiwa ni kufika fainali, tunaamini hicho ni kitu kinachowezekana.

Hakuna ubishi kuwa Simba kwa sasa inaonekana kukamilika kila idara na imesheheni wachezaji wenye vipaji ambao wanaweza kuamua matokeo wao binafsi wakati pindi mipango, mbinu na ufundi wa kocha unapokwama uwanjani, jambo ambalo linatufanya kuamini timu hiyo inaweza kufika fainali kama tu dhamira na kiu hiyo itaingia akilini mwa wachezaji.

Na kwa upande wa Namungo ambayo inaipeperusha bendera ya Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho, tayari imetinga hatua ya makundi baada ya kupata matokeo ya jumla ya mabao 7-5 katika mechi mbili za mchujo dhidi ya CD de Agosto ya Angola.

Kwa Namungo kufika tu hatua hiyo, ni mafanikio makubwa kwake, kwani tayari imeweka rekodi kwa kuwa klabu ya kwanza Tanzania kushiriki michuano hiyo kwa mara ya kwanza na kufanikiwa kufika hatua ya makundi.


Lakini kuitoa timu kongwe kama De Agosto, huo ni ujumbe tosha kwa wapinzani wao kwenye hatua ya makundi kujiandaa vizuri kabla ya kukutana wakati huu Namungo ikijiandaa kwenda Morocco kuivaa Raja Casablanca Machi 10, mwaka huu.

Namungo ambayo ipo Kundi D pamoja na Raja Casablaca ya Morocco, Pyramids (Misri) na Nkana ya Zambia, kwa hakika ni moja kati ya kundi gumu na lenye timu kongwe na zoefu kwenye michuano hiyo ya Afrika.

Ingawa halitakuwa kundi jepesi kwake kuweza kufurukuta, sisi tunaamini hakuna kinachoshindikana uwanjani kama wachezaji na benchi la ufundi la Namungo watajipanga huku uongozi ukihakikisha unamaliza masuala yote ya nje ya uwanja.

Tunapata imani zaidi kwa Namungo kuweza kufanya vizuri na kufika mbali hasa tukitumia kigezo cha kuweza kuibuka na ushindi wa mabao 6-2 katika mechi ya kwanza dhidi ya De Agosto, timu ambayo ni kongwe na kigogo katika michuano hiyo ya Afrika, hivyo huu ni mwaka ambao Watanzania wanatarajia mafanikio makubwa kwenye michuano hiyo ya CAF kutoka kwa timu hiyo pamoja na Simba.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Ngoma ikivuma sana hupasuka

Na Barnabas Maro

**NGOMA** ivumayo sana kutokana na kupigwa huishia kupasuka. Hii ni methali inayotumiwa kutukumbusha kwamba jambo lolote huharibika hasa linapopita kipimo chake. Wengine husema "Ngoma ya kuvuma vuma haikawi kupasuka."

Niliuona mchezo baina ya Simba ya Tanzania na Al Ahly ya Misri uliochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa pale Temeke jijini Dar es Salaam Jumanne iliyopita.

Mpaka kipindi cha kwanza kilipomalizika, bado nilikuwa siamini macho yangu kwa niliyoyaona uwanjani! Al Ahly ndio bingwa iliyotwaa Kombe la Afrika mara nne mfululizo ilhali Simba ya Tanzania haijafika hata nusu fainali katika kuwania kombe hilo linaloshindaniwa na timu za nchi mbalimbali barani Afrika.

Mchezo ulivyokuwa kipindi cha kwanza, nilidhani Al Ahly ilileta timu ya pili kwa kuidharau Simba, kumbe sivyo. Ilikuwa timu iliyokamilika. Mshangao wangu wa kwanza ukaanzia hapo! Hii ndio Al Ahly inayotambulika si Afrika tu bali hata Ulaya? Ni kweli ngoma ikivuma sana hupasuka. Ndiyo hiyo Al Ahly!

Mshangao wangu wa pili ulikuwa kwa wachezaji wa Simba kwa namna walivyocheza siku ile! Nikajiuliza kimoyomoyo: "Kama mchezo wake (Simba) ndiyo huu, mbona kwenye ligi yetu imepoteza michezo miwili na kwenda sare mara tatu?"

Uchezaji wao wa siku ile ulinipa wasiwasi kama kuna timu itakayomudu uchezaji wa Simba na kwa sababu hiyo, njia ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu kwa mara ya nne mfululizo ipo wazi kwao. Anayebisha lakini ndivyo nionavyo mimi.

Wenzangu wa upande ule waliokuwa wakiwashangilia Waarabu ambao wapo juu kabisa kwenye Bara la Afrika wakapigwa na butwaa, yaani mshangao mkubwa, bumbuwazi. Wakatulia tuli kama maji mtungini.

Niliifahamu Sandalendi (Sunderland) tangu mwaka 1962 nilipokuja Dar es Salaam na kuwa makazi yangu mpaka sasa lakini sijapata kuiona Sunderland ambayo sasa yaitwa Simba, kama ilivyoikabili Al Ahly na kufanya timu hiyo ya Arabuni kudhibitiwa kila pembe huku wachezaji wa Simba wakicheza kama wapo mazoezini!

Wachezaji wa Al Ahly walipoteza mwelekeo na kuonekana kama wanaofunzwa na wenzao wa Simba ya Msimbazi, Dar es Salaam!

Hapa nikawakumbuka wahenga waliosema: "Hakuna mume wa waume." Maana yake hakuna mtu mmoja anayeweza kuwashinda wanaume wenzake wote. Hii ni methali ya kutumiwa kwa mtu anayejitia ubabe au anayejidai kuwa na nguvu kama njia ya kumnyamazisha.

Kwa mchezo aliyocheza Simba, hata huko ugenini kwenye mechi ya marudiano, naona Al Ahly itapigwa, tena kwa zaidi ya bao moja walilopigwa jijini Dar es Salaam!

'Chuki' ni hisia ya kutopenda kitu au jambo. Hali ya kutokuwepo upendo, hali ya kuwa na roho mbaya, hali ya kuwa na kinyongo. Yanga na Simba ndizo timu za kwanza kuanzishwa kati ya timu zilizopo hapa nchini. Ajabu ni kwamba hata zinapocheza mkoa wowote humu nchini hushangiliwa zaidi na watu wa mikoa hiyo badala ya kuzishangilia timu za mikoa yao!

Kwa Yanga na Simba mambo ni tofauti. Timu yoyote kati ya hizi mbili zinapocheza na timu kutoka ughaibuni, yaani nje ya Tanzania, timu ngeni hushangiliwa kwa hoihoi, yaani kwa sauti ya furaha, shangwe na nderemo za kushangilia moja wapo inapofungwa na timu ngeni ya ughaibuni! Ujinga ulioje?

Yanga na Simba ni watoto wa mama mmoja aitwaye Dar es Salaam na baba mmoja aitwaye Tanzania. Kama ndivyo, kwa nini tuchukiane na kudhuriana wenyewe kwa wenyewe?

"Udugu wa nazi hukutania chunguni." Methali hii hutumiwa kuwapigia mfano watu (hasa Yanga na Simba) wasioweza au wasiopenda kushirikiana!

Ukisikiliza maneno wasemayo mashabiki wa Yanga na Simba utadhani si timu za jiji na nchi moja ingawa mwanzoni zilikuwa moja! Ikumbukwe kuwa neno analolitamka mtu ni kama mkuki, likitoka halirudi na huweza kuleta madhara.

Twapaswa kuwa na tabia ya kuyatafakari maneno tuyasemayo kabla. Ni vizuri kulipima neno kabla ya kulisema na kujiletea majuto baadaye. Yasikitisha kwamba Yanga na Simba zachukiana kama mbwa na paka ilhali walizaliwa wakati mmoja tena kwenye mkoa mmoja- Dar es Salaam!

"Damu ni nzito kuliko kitarasa." Kitarasa ni aina ya ndizi ambayo hutoa utomvu mwekundu. Kwa hiyo damu haiwezi kufanana na kitarasa. Methali hii inatufunza kwamba uhusiano wa kidamu ni muhimu sana.

Yanga na Simba ni wazaliwa wa jiji moja, mkoa mmoja na nchi moja iliyoshiriki kwenye ukombozi na uhuru wa nchi mbalimbali za Afrika. Chuki baina ya Yanga na Simba inaleta maana gani?

**marobarnabas@yahoo.com 0784-334 096**

# TASAF kuzifikia kaya milioni 1.4

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

AWAMU ya tatu ya kunusuru kaya maskini chini ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), inatarajia kuzifikia zaidi ya kaya milioni 1.4 zinazokadiriwa kuwa na watu zaidi ya milioni saba kote nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Ladislaus Mwamanga, alisema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya siku sita ya timu maalum ya wawezeshaji 25 kutoka halmashauri za Madaba na Songea yaliyofanyika kwenye ukumbi wa Ushirika mjini hapa.

Mwamanga alisema wawezeshaji hao watahusika na utekelezaji na usimamizi wa miradi ya kutoa ajira za muda kwa walengwa wa mpango wa kunusuru kaya maskini wa TASAF Awamu ya Tatu katika kipindi cha pili.

"Miradi ya kutoa ajira za muda inalenga kutoa ajira kwa kaya maskini wakati wa kipindi kigumu ili wanakaya hao wasiuze rasilimali walizo nazo kwa ajili ya kupata fedha na kuwezesha ajira kwa kaya ili kuongeza kipato, hivyo kupunguza umaskini," alisema.

Hata hivyo, alizitaja kaya zitakazoshiriki utekelezaji wa miradi hiyo ni zenye watu wenye uwezo wa kufanya kazi na wenye umri wa kuanzia miaka 18 hadi 65.

Mwamanga alisema katika kipindi cha kwanza cha mpango wa kunusuru kaya maskini, miradi 9,440 ya kutoa ajira za muda ilitekelezwa kwa gharama ya Sh. bilioni 1.19 na kati ya hizo, Sh. bilioni 83.3 zilitumika kwa kulipa ujira wa walengwa na Sh. bilioni 35.7 kwa ajili ya vifaa vya miradi na usimamizi.

Mwezeshaji wa Mafunzo hayo kutoka TASAF makao makuu, Frank Antony, alisema lengo la mafunzo hayo ni kujenga uwezo wa timu za wataalamu ngazi ya halmashauri za Songea na Madaba kuhusua uibuaji, uandaaji, utekelezaji na usimamizi miradi ya kutoa ajira za muda kwa walengwa ngazi ya jamii.

Alisema mafunzo hayo ya nadharia na vitendo ya siku sita ambayo yametolewa kwa wawezeshaji 25, yatawapelekea maarifa walengwa 5,400 wa TASAF kati yao walengwa 3,800 toka Halmashauri ya Songea na 1,600 toka Madaba.

"Baada ya mafunzo haya, tunategemea wawezeshaji watakwenda kuwasaidia walengwa ngazi ya jamii kuibua miradi ngazi ya jamii yenye tija na itakayoonyesha thamani ya fedha,'' alisisitiza Antony.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Athuman Nyange, aliitaja miradi iliyotekelezwa katika kipindi kilichopita kuwa ni uboreshaji wa visima vya asili, ujenzi wa vivuko vya watembea kwa miguu, uchimbaji mabwawa ya samaki na uanzishwaji vitalu vya miche ya miti.

# Makandarasi wazawa wazembe kutopewa kazi miradi ya maji

**Na Neema Emmanuel,** SENGEREMA

SERIKALI imetangaza kuwanyima kazi makandarasi wazawa ambao wameshindwa kutekeleza miradi ya maji kwa wakati, hivyo kukwamisha lengo la serikali la kumtua ndoo mama kichwani.

Hayo yalibainishwa jana wilayani hapa na Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, wakati wa ziara ya kukagua mradi wa maji katika vijiji vya Buyagu, Kalangalala, Bitoto, Mwalinga, Nyamagana, Magulukende, Bukokwa na Nyampande.

Alisema makandarasi wazembe hawatapewa kazi za miradi ya maji na kutolea mfano kampuni ya D4N Construction Limited ya wilayani Kahama ambayo ilishindwa kukamilisha mradi wa Buyagu, Kangalala na Bitoto kwa mujibu wa mkataba.

Mahundi alisema mkandarasi huyo alipewa Sh. bilioni 1.7 na kuanza kutekeleza mradi huo Desemba, 2013 na ulipaswa kukamilika Juni, 2014.

"Mkandarasi amekaa na kazi miaka saba, kazi imemshinda na ukiangalia ubora wa kazi yake ni mbovu. Huyo D4N aandike kwamba kwenye wizara yetu hatapata kazi yoyote," alisema Mahundi.

Aliongeza kuwa walimpatia fedha aanze kazi lakini alizitumia kutatua matatizo yake na familia yake, hivyo makandarasi wote wajanja na wazembe, hawatapata nafasi kwani lengo la serikali la kuwapa kazi ili kuwahudumia wananchi lakini inasikitisha baada ya kufanya kinyume. "Mkandarasi mzembe atapokonywa mradi na atawekwa kwenye orodha ya makandarasi ambao hawana sifa ya kukabidhiwa kutekeleza miradi ya maji kote nchini," alisema.

Awali akiwasilisha taarifa ya mradi huo uliokwamishwa na D4N, Meneja wa Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Sengerema, Cassian Wittike, alisema mradi huo ulikuwa miongoni mwa miradi ya vijiji 10 chini ya mpango wa maendeleo katika sekta ya maji kwenye programu ndogo ya maji na usafi wa mazingira vijijini.

Wittike alisema uwezo mdogo wa mkandarasi na kuchelewa kwa malipo ya IPC ndiyo chanzo cha kutokamilika mradi huo kwa wakati hivyo baada ya RUWASA kukabidhiwa waliweza kusimamia utekelezaji wake na kuukamilisha.

Alisema wananchi wa kijiji cha Buyagu wanapata huduma ya maji kwa vituo 15 pia kukamilika kwa mradi huo utawanufaisha zaidi ya wananchi 16,000.

Meneja huyo aliongeza kuwa miradi yote imefikia asilimia zaidi ya 75 na kwamba kufikia Machi, mwaka huu, itakamilika na zaidi ya wananchi 95,000 watanufaika.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama (wa nne kushoto), akiangalia mabwawa yanayojegwa katika mradi wa kiwanda cha machinjio ya kisasa cha Ranchi ya Nguru Hills, kwa ajili ya kupokea maji kutoka kwenye machinjio na kutibiwa kabla ya kutumika kwenye kilimo cha umwagiliaji, alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi huo, Mvomero, mkoani Morogoro juzi. **PICHA: OWM**

# Washangaa waliotafuna fedha kuachiwa

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

BAADHI ya wananchi mkoani Rukwa wamesikitishwa na kitendo cha kutochukuliwa hatua mpaka sasa baadhi ya watendaji wa serikali wanaotuhumiwa kula fedha za makusanyo ya mapato ya halmashauri, hali waliyodai inawakatisha tamaa kulipa tozo na kodi mbalimbali.

Wananchi hao walisema hayo juzi, kwa nyakati tofauti baada ya kusikia Mkuu wa Mkoa huo, Joachim Wangabo, ametoa siku 14 wawe wamerudisha Sh. milioni 932 vinginevyo watafikishwa mahakamani.

Mmoja wa wananchi hao, Furaha Kabinda, mkazi wa wilayani Nkasi, alisema anasikitika kuona watuhumiwa hao hawajafikishwa mahakamani ili wakajibu tuhuma dhidi yao.

"Nimeshtuka sana kusikia suala hili kama bado halijaisha, maana tangu nimeanza kulisikia ni zaidi ya mwaka sasa. Kitendo hiki ni kucheza na maendeleo ya wananchi, sisi tunalipa kodi ili tupate maendeleo, baadhi ya watendaji wa serikali wanakula fedha hizo. Huku ni kucheza na maisha yetu," alisema.

Naye Flaviana Kilosa, mkazi wa Sumbawanga Mjini, alisema kitendo hicho kimemsikitisha kwa kuwa watuhumiwa wa wezi walioko mitaani wanakamatwa na kufikishwa mahakamani haraka, lakini watendaji wa serikali wanabembelezwa kurejesha fedha za umma hii si sawa.

"Pamoja na kuwa watuhumiwa hao wamefikishwa TAKUKURU (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa) walipaswa wafikishwe mahakamani upesi ili wananchi tuone hatua zinachukuliwa haraka kwani kumekuwapo na hisia kwa kuwa ni mali ya umma ndiyo maana kuna kusuasua na hii inawakatisha tamaa walipakodi," alisema. Hivi karibuni, Wangabo alitoa siku 14 kwa watendaji wa serikali na watu waliokuwa mawakala wa kukusanya mapato katika halmashauri zote nne za mkoa huo wanaodaiwa kula fedha mbichi za serikali, warejeshe vinginevyo atawaagiza TAKUKURU kuwafikisha mahakamani.

Alisema mkoa huo uliweka makisio ya kukusanya Sh. 9,487,289,000 katika mwaka wa fedha wa 2020/21, lakini mpaka nusu ya kwanza ya mwaka, umekusanya Sh. 3,682,531,918.16, sawa na asilimia 38.8 tu.

HABARI KITAIFA

## NMB yatoa msaada mil. 18.5/- elimu, afya

**Na Christina Haule,** MVOMERO

BENKI ya NMB Kanda ya Mashariki imetoa msaada wa vitu mbalimbali kwa sekta za elimu na afya wilayani hapa vyenye thamani ya Sh. milioni 18.5.

Meneja wa NMB Kanda ya Mashariki, Dismas Prosper, alisema hayo jana wakati akikabidhi vifaa hivyo yakiwamo madawati 50 kwa ajili ya Shule ya Msingi Mkindo B, viti 40 na meza 40 kwa ajili ya Shule ya Sekondari Diongoya.

Pia katika misaada hiyo, yamo magodoro manane, vitanda vinane na mashuka 50 kwa ajili ya hospitali ya Turiani - Bwagala na mabenchi 20 ya Kituo cha Afya cha Kibati.

Prosper alisema kwa zaidi ya miaka 10, mfululizo wamekuwa wakichangia asilimia moja ya faida yao ya kila mwaka kama sehemu ya uwajibikaji kwa jamii inayowazunguka.

Alisema NMB ndiyo benki inayoongoza kwa kuwa na matawi mengi nchini na mpaka sasa ina matawi 226, zaidi ya ATM 800, zaidi ya mawakala 8,000 na idadi ya wateja zaidi ya milioni nne idadi ambayo alisema ni hazina kubwa kulinganisha na benki zingine.

Kwam ujibu wa Prosper, NMB imezifikia wilaya zote nchini kwa asilimia 100 na inaendelea kuboresha huduma za kibenki kwa njia za mitandao ili kufikisha huduma za kibenki kwa wananchi wengi zaidi. “NMB ni sehemu ya wananchi wote sababu wao wameonesha mchango mkubwa katika kuendesha benki, hivyo haina budi kuchangia maendeleo kupitia nyanja mbalimbali za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja,” alisema.

Prosper alisema NMB itaendelea kuunga mkono juhudi za wadau wake wakubwa katika kuhakikisha changamoto za jamii zinapatiwa ufumbuzi katika kujenga afya bora kwa jamii ya Watanzania.

Akipokea thamani hizo Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Albinus Mugonya, aliiomba NMB kutowachoka kwa maombi yao ya mara kwa mara yenye lengo la kuunga mkono juhudi za Serikali ya awamu ya Tano katika sekta za elimu na afya na kwenye majanga.

Alisema NMB imeonyesha mwitikio katika mambo mbalimbali wilayani hapa ikiwamo walipopata mafuriko kwenye tarafa ya Mlali yaliyosababisha wakazi kukosa makazi na sasa wanasaidia vifaa vya shule na hospitali.




Mafundi wakiendelea na ujenzi wa miundombinu ya mabasi ya mwendokasi kuanzia Mbagala hadi Gerezani, katika eneo la Kurasini, barabara ya Kilwa, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Waziri awapigia debe ajira vijana mradi maji

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAZIRI wa Maji Jumaa Aweso, amemtaka mkandarasi anayetekeleza ujenzi wa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria katika mji wa Tinde wilayani Shinyanga na Shelui mkoani Singinda, kuwapa ajira vijana wa maeneo hayo.

Aweso alisema hayo juzi katika mji mdogo wa Tinde wakati wa kutia saini mkataba wa ujenzi wa mradi huo ambao utatekelezwa na kampuni ya Megha Engineering Construction ya India, wenye thamani ya Sh. bilioni 24.4.

Kwa mujibu wa Aweso, mradi huo utajengwa miezi 12 na utakapokamilika utawahudumia wananchi wa Tinde na Shelui.

“Vijana ambao mtapewa vibarua kwenye utekelezaji wa mradi huu, naombeni muwe waaminifu. Msihujumu mradi wala kuiba vifaa vya ujenzi bali fanyeni kazi kwa uaminifu na kujipatia kipato,” alisema Aweso.

“Mradi huu ni muhimu sana kwa wananchi wa Tinde na Shelui ambao utawaondolea adha ya kufuata maji safi na salama umbali mrefu pamoja na kupoteza muda wa kufanya shughuli za kimaendeleo,” aliongeza.

Aweso alitoa tahadhari kwa mkandarasi huyo anayetekeleza mradi huo kuwa hiyo kazi yake ya kwanza na kwamba akiwa Waziri wa Maji, hataki ubabaishaji bali afanye kazi na kuimaliza kwa wakati.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Anthony Sanga, ambaye ndiye aliyetia saini mkataba huo pamoja na mkandarasi, alisema fedha za utekelezaji wa mradi huo ni mkopo wa masharti nafuu kutoka nchini India kupitia benk ya Exim.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, alimshukuru Rais John Magufuli kwa kutekeleza ahadi yake ya kupeleka huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wa Tinde na Shelui.

Alisema serikali itatoa ushirikiano kwa mkandarasi huyo ili asipate vikwazo vyovyote wakati wa utekelezaji.

## Naibu Waziri asisitiza utalii ndani kuongeza pato la taifa

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, amesisitiza kuwa fursa zilizoko kwenye sekta ya utalii zikitumika ipasavyo, zitasaidia kukuza pato la taifa na uchumi wa mtu mmoja mmoja.

Masanja alisema hayo jana, jijini hapa, wakati wa kikao cha pili cha Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Mwanza kwa mwaka 2020/21.

Alisema takwimu za watalii wanaoingia nchini mwaka 1993 walikuwa 230,000 lakini hadi mwaka 2019, waliongezeka hadi kufikia milioni 1.5. “Idadi ya Watanzania kwa sasa ni milioni 60 lakini ukingalia takwimu hizo watalii wanaoingia kwenye hifadhi zetu kuangalia vivutio ni milioni 1.5. Hii inaonyesha Watanzania tuna kazi kubwa ya kufanya, kuwa wazalendo na kupenda vile tulivyo navyo,” alisema.

Katika hatua nyingine, Masanja amewaeleza viongozi wa Mkoa wa Mwanza kuwa uwepo wa vivutio vingi vya utalii katika Kanda ya Ziwa ni fursa pekee ya wananchi kuendelea kunufaika.

“Ni lazima tuongeze nguvu katika kuhamasisha utalii wa ndani bila kusahau kuhamasisha wageni kutoka nje ya nchi yetu. Utalii wa ndani unatuhusu sisi wenyewe. Nikiuliza hapa wangapi wamefika kwenye hifadhi zetu na kwenye vivutio mbalimbali tulivyo navyo, tutabaini idadi kidogo sana, nawaomba sana tuhamasishane,” alisema.

Hata hivyo, alisema janga la Corona limesababisha kuyumba kwa sekta utalii duniani kote pia hapa nchini kwa kuwa watalii waliokuwa wakitegemewa, nchi zao zimeathiriwa, hivyo ni wajibu wa kila Mtanzania kuwa balozi wa kutangaza utalii na kutembelea vivutio vilivyopo.



# RC ataka kasi ujenzi mradi wa maji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKALA wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), umeagizwa kuongeza kasi ya ujenzi wa mradi wa maji wa kijiji cha Mtera wilayani Mpwapwa ili wananchi waondokane na adha ya kutumia maji ya chumvi.

Ujenzi wa mradi huo uliagizwa na Rais John Magufuli, Septemba mwaka jana, baada ya wananchi wa eneo hilo kumwomba kupatiwa maji baridi kutokana na kutumia maji ya chumvi kwa muda mrefu.

Akikagua ujenzi wa mradi huo jana, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alisema mradi huo unapaswa kukamilika kwa wakati ili wananchi hao waondokane na adha hiyo.

"Uwapo wa miundombinu na huduma za kijamii kama maji na umeme kutaongeza tija na kukuza uchumi wa Mji wa Mtera ambao upo karibu na bwawa la Mtera, kuchelewa kwa mradi huo ni kurudisha nyuma juhudi za kuinua maisha ya wakazi wa Mtera," alisema.

"RUWASA mmefanya kazi nzuri, lakini mnahitaji kuongeza kasi ili wananchi wa mji huu wapate huduma ya majisafi na salama, uwepo wa maji utavutia uwekezaji mwingine ikiwamo vituo vya afya na biashara nyingine," aliongeza.

Mkuu huyo pia aliitaka RUWASA kuhakikisha maji yanafika katika Kituo cha Afya Chipogoro ambacho ujenzi wake ulianza baada ya Rais Magufuli kutoa fedha mwaka jana ili kuboresha huduma za afya kwenye eneo hilo.

"Kituo kile ni msaada mkubwa kwa wasafiri wa barabara hii kubwa, hivyo maji lazima yafike pale mapema ili hata madaktari wasishindwe kuishi pale kisa ukosefu wa maji," alisema.

Meneja RUWASA wa Wilaya ya Mpwapwa, Mhandisi Cyprian Warioba, alisema mradi huo utekelezaji wake ulianza Desemba, mwaka jana na unatarajiwa kukamilika mwezi Aprili badala ya Machi 15, mwaka huu kama ilivyopangwa awali.

Naye Meneja wa RUWASA Mkoa wa Dodoma, Dk. Godfrey Mbabaye, alisema mradi huo umegawanyika katika awamu mbili. Ya kwanza ni ya muda mfupi ambayo inakaribia kukamilika na ya pili ni ya muda mrefu ambayo bado haijaanza.



Mbunge wa Chamwino, Deogratius Ndejembi (mbele), akikagua ujenzi unaoendelea wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Sekondari ya Itiso, wilayani Chamwino, mkoani Dodoma juzi, kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza waliokosa nafasi kuingia darasani kwa sababu ya upungufu wa madarasa. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Maofisa maendeleo watakiwa kuacha mazoea

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu, Wizara ya Afya, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu, amewataka maofisa maendeleo ya jamii nchini, kuwa wabunifu na kuacha kufanya kazi kwa mazoea.

Dk. Jingu aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akiwasilisha mada kuhusu umuhimu wa uongozi wa kimkakati kwenye Kongamano la Chama cha Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (CODEPATA).

"Maofisa maendeleo ya jamii mnatakiwa kuwaza zaidi, kuwa wabunifu na kufikiria namna bora ya kufanya mambo katika mwonekano tofauti.

Huo ndio uongozi wa kimkakati vinginevyo inakuwa kufanya kazi kwa mazoea," alisema.

Katibu Mkuu pia aliwahimiza kuwa na uongozi wa kimkakati unaoleta mabadiliko katika nyanja husika.

"Ofisa Maendeleo ya Jamii ni mtu wa kuchochea mabadiliko katika eneo alilopo na kama kiongozi wa kimkakati lazima uwe na mambo kadhaa ikiwamo kuwa na dira au lengo mahususi, mahitaji ya kufikia lengo, jinsi ya kufikia lengo na tathmini ya kina ya mazingira waliyopo," alifafanua.

Dk. Jingu alisisitiza kujifunza namna ya kuwasilikiza walengwa, kujenga timu ya ushirikiano kiutendaji na kuzingatia misingi ya uadilifu ilivyo katika miongozo ya watumishi wa umma.

Akichangia mada hiyo, mmoja wa washiriki, Moses Kisibo, alisema kuwa umuhimu wa kuwapo kongamano la aina hiyo mara kwa mara ili kuleta ufanisi kwenye kada hiyo.

# Wakulima wafundwa kuhusu bima ya mazao

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imewataka wakulima kutumia bima ya mazao ili kuepuka athari na hasara zinazotokana na majanga mbalimbali ikiwamo mafuriko na ukame.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, alitoa rai hiyo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa baada ya mkutano wa mafanikio ya kilimo cha umwagiliaji kati Tanzania na wadau wa kilimo kutoka Japan.

Kusaya alisema ni wakati muafaka sasa wakulima kuhakikisha katika mazao waliyolima yanakuwa na bima.

"Unapokuwa na bima unakuwa na uhakika pale inapotokea mafuriko una uhakika wa kupata fidia au kutokea ukame wa kupitiliza na kuathiri mazao basi unakuwa na uhakika wa kupata fidia," alisema.

Katibu huyo alisema mtu atalipwa fidia kulingana na alichopoteza kutokana na athari hizo hivyo ni vyema kuwa na bima ya mazao.

Kaimu Mkurugenzi, Uratibu Sekta katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Enock Nyanda, alisema ofisi hiyo inashirikiana na mamlaka za serikali za mitaa ili kukuza kilimo cha umwagiliaji.

"Tunashirikiana na wenzetu Wizara ya Kilimo na mamlaka za serikali za mitaa ili zitenge kiasi cha fedha kutokana na mapato yake ya ndani ili kuwezesha ujenzi wa miradi midogo ya umwagiliaji," alisema.

Pia alisema hatua hiyo itasaidia kilimo hicho kufanyika katika mzunguko wa mwaka mzima.



# Wizara yajipanga ukarabati visima

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Maji na Nishati imesema visima 69 vilivyojengwa kupitia mradi wa Rasilhema, vitafanyiwa ukarabati ili kutoa huduma vizuri kwa wananchi.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Maji na Nishati, Suleiman Masoud Makame, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Wawi, Bakari Hamad Bakari, aliyetaka kujua maendeleo ya visima vya mradi wa Rasilhema vikoje kwa sasa.

Alisema baadhi ya visiwa vinatoa huduma na kupunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la majisafi na salama kwa wananchi wa maeneo mbalimbali Unguja na Pemba.

Pia alisema imebainika baadhi ya visima vilivyochimbwa kupitia mradi huo, havifanyi kazi na wizara iko katika mpango wa kuvifanyia ukarabati ili kuzalisha maji.

"Mheshimiwa Spika visima 69 vimechimbwa katika mradi wa Rasilhema, lakini baadhi havifanyi kazi. Wizara inakusudia kuvifanyia ukarabati tena ili kutoa huduma kwa wananchi," alisema.

Kadhalika, alisema tatizo la majisafi na salama kwa baadhi ya maeneo ikiwamo Mjini Magharibi linatazamiwa kupatiwa ufumbuzi kutokana na utekelezaji wa mradi wa maji kutoka India.

Alisema mradi huo ni muhimu kwa wananchi wa mkoa wa Mjini Magharibi na sehemu zingine na utekelezaji wake kwa kiasi kikubwa utakuwa ufumbuzi wa tatizo la upatikanaji wa majisafi na salama.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Dk. Khalid Salum Mohamed, akijibu swali wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Awashukia watendaji migogoro ya ardhi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdalla, amewataka watendaji wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kuzipatia ufumbuzi kesi za migogoro ya ardhi ambayo imesababisha wananchi wanyonge kudhulumiwa haki ya umiliki.

Suleiman alisema hayo jana wakati akiahirisha kikao cha Baraza la Wawakilishi huku akisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imejipanga na kuzipatia ufumbuzi vikwazo vyote vinavyokwamisha maendeleo ya wananchi.

Alisema kuna ongezeko kubwa la migogoro ya ardhi ambayo baadhi imekuwa ikichangiwa na viongozi, hivyo kushindwa kupata haki zao wanazostahiki.

Hemed alisema kwa kila mwananchi anayo haki ya kumiliki ardhi kwa matumizi mbalimbali kwa mujibu wa sheria na watendaji wa ardhi watakaobainika kujishughulisha na vitendo hivyo, watachukuliwa hatua za kisheria.

"Mheshimiwa Spika, tunapenda kuwatahadharisha watendaji katika sekta ya ardhi kwamba serikali haitavumilia na wahusika wote watakaobainika kujishughulisha na matukio hayo, watachukuliwa hatua za kisheria," alisema.

Pia alisema SMZ imejipanga kudhibiti uvujaji wa mapato kwa kuanzisha mfumo mpya wa kufanya malipo kwa njia ya kielektroniki na kuachana na utaratibu uliozoeleka wa kufanya malipo kwa njia ya kutoa risiti za mikononi.

Makamu wa Pili wa Rais aliwataka wafanyabiashara na wananchi wawe tayari kulipa kodi kwa hiari na kuepuka usumbufu, huku akiwataka wananchi wanaofanya ununuzi wawe tayari kudai na kuchukuwa risiti.

Alisema wako wafanyabiashara wanauza bidhaa mbalimbali, lakini hawatoi risiti na kusema kitendo hicho ni kosa kwa mujibu wa sheria kwa sababu lengo lake ni kuikosesha serikali mapato.

"Mheshimiwa Spika, moja ya maeneo ambayo serikali inapoteza mapato yake mengi ni kitendo cha wafanyabiashara kukataa kutoa risiti na wananchi wenyewe kushindwa kudai risiti," alisema.

Pia alisema Serikali ya Zanzibar itaendelea na mapambano dhidi ya rushwa na kuwataka watumishi wa serikali wakiwamo wanaofanya kazi katika sekta za fedha kubadilika na watendaji watakaobainika kujishughulisha na matukio hayo, watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Alisema tayari Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA) imefanya kazi kubwa katika kuchunguza tuhuma mbalimbali na matokeo yake yameonekana kwa wananchi wote ikiwamo kurudisha fedha za umma zilizokuwa zikishikiliwa na viongozi kinyume cha sheria.

"Tunaipongeza kwa dhati ZAECA kwani imefanya wamefanya kazi kubwa ya kufichua uovu na ubadhirifu unaofanywa na watumishi wasiokuwa waaminifu," alisema.

Katika kikao cha wiki mbili cha Baraza la Wawakilishi, wajumbe walipokea taarifa mbalimbali muhimu ikiwamo ripoti ya ZAECA, ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

# Barabara kwenda kaburi la Dk. Omar kukarabatiwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imesema barabara yenye urefu wa kilomita moja kuelekea maeneo ya makaburi ya aliyekuwa Makamu wa Rais wa Muungano, Dk. Omar Ali Juma, itafanyiwa ukarabati ikiwa sehemu ya kuwaenzi viongozi wakuu wa serikali kwa mujibu wa sheria.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Dk. Khalid Salum Mohamed, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Wawi, Bakari Hamad Bakari.

Katika swali lake hilo, Bakari alitaka kujua lini barabara ya kuelekea katika kaburi ya Dk. Omar itafanyiwa ukarabati.

Dk. Mohamed alisema SMZ imepitisha sheria ya kuwaenzi viongozi wakuu wa serikali kwa lengo la kutunza kumbukumbu mbalimbali za viongozi hao.

Alisema Dk. Omar Ali Juma, ambaye sasa ni marehemu, mchango wake kwa upande wa Zanzibar ni mkubwa na atakumbukwa kutokana na utumishi wake akiwa Waziri Kiongozi wa SMZ mwaka 1988 hadi 1995.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tumepitisha sheria ya kuwaenzi viongozi wakuu wa serikali wa kitaifa ambapo utekelezaji wake unafanyika kwa mujibu wa sheria. Barabara inayoelekea katika kaburi la kiongozi wetu, marehemu Dk. Omar Ali Juma, itafanyiwa ukarabati," alisema.

Katika uhai wake, Dk. Omar alikuwa Makamu wa Rais wa Tanzania mwaka 1995 hadi 2001 chini ya Rais Benjamin Mkapa (naye sasa marehemu) hadi alipofariki dunia na nafasi yake kuchukuliwa na Dk. Ali Mohamed Shein.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
DANI
TELE



**UJU HONGERA YAKO KUMILIKI NDINGA KALI** Uk.14

JUMAMOSI FEBRUARI 27, 2021



# Wapo kwenye orodha

MLOLONGO wa wasanii wa filamu kujihusisha kimapenzi na wanamuziki wa Bongo Fleva, unazidi kuongezeka baada ya Msami kutaja orodha ya waigizaji wa kike aliotoka nao kimapenzi.

Si jambo geni kwa wanamuziki wa kiume kujihusisha kimapenzi na wasanii wa kike wa filamu, lakini kitu kinachowashangaza wengi ni jinsi mapenzi hayo yanapogeuka mwiba pale yanapokwisha.

Sasa imekuwa jambo la kawaida kwa wanamuziki wa kiume kuweka hadharani wanawake aliotoka nao kimapenzi ikiwamo waigizaji kama njia ya kuongeza umaarufu.

Jana mwanamuziki Msami, naye aliwataja wasanii wawili wa filamu ambao kwa nyakati tofauti alikuwa katika uhusiano wa kimapenzi.

Waigizaji waliotajwa ni Irene Uwoya na Kajala Masanja, akiwaelezea kama wanawake waliomwingiza katika mapenzi licha ya umri wake kuwa mdogo.

Msami amesema wakati akiwa katika mapenzi na Kajala hawakufikia hatua ya kuanza kuchorana tatoo.

Aidha, alimtaja Uwoya kuwa ndiye mwanamke aliyewahi kuwa naye kwenye uhusiano na kutaka kumchora tattoo, lakini hafahamu kama yeye alichorwa au la.

"Wanaocheka umri au kipato kwenye uhusiano wao hawajui maana ya mapenzi, mimi nawapongeza sana Harmonize na Kajala nawaombea wafikie malengo yao pia mimi ni shabiki yao napenda uhusiano wao, nataka kuona wakifika mbali zaidi," amesema.

Harmonize na Kajala kwa sasa wapo katima mapenzi mazito na wote wawili waliweka wazi uhusiano wao hivi karibuni baada ya kuwepo uvumi kwa muda mrefu.

Wasanii wengine wa muziki ambao walikuwa na uhusiano wa kimapenzi na waigizaji wa kike ni Diamond Platnumz ambaye alikuwa na Wema Sepetu na Hamisa Mobeto.

Pia rapa Nay wa Mitego alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Shamsa Ford.

## BASI SAWA

## 20 Percent hataki umbea

MSANII wa muziki wa Bongo Fleva ambaye anapigania kurudi katika gemu, 20 Percent, amesema huwa anachukizwa pale anapotakiwa kuwajadili wasanii wengine.

Amesema maswali anayoulizwa kuhusu wasanii Alikiba na Harmonize, yanampa tabu kujibu kwa sababu sio kitu muhimu kwake na mashabiki zake.

"Nakasirishwa kuongeleshwa mambo mengi yasiyonihusu hata kama nikija na kazi zangu mkononi nitaulizwa kuhusu fulani na fulani, kwa mfano unaulizwa kuhusu Alikiba au Harmonize kitu ambacho pengine sio muhimu kwa mashabiki zangu," amesema




## Chidi Benz akubali 'Kiki' Bongo Fleva

RAPA Chidi Benz, ameshangaa wanaohoji kuhusu matukio ya kiki, akisema mitandao ya kijamii inawalazimisha wasanii kuelekea upande huo.

Akizungumzia hilo kwenye shoo ya Planet Bongo ya East Africa Radio, Chidi Benz amesema huwa anapata tabu kusikia watu hawataki suala hilo, kwani wao wanalazimishwa kutumia mbinu hizo ili kupata mashabiki kwa wingi.

"Sijaelewa kwanini watu hawataki kiki na wanajua kabisa tupo wakati wa kiki, twende mbele turudi nyuma Ulimwengu wa sasa ni kiki, mitandao haiwezi kuwa mingi halafu kusiwe na kiki, inapoteza kwa sababu watu wengine wanaangalia zaidi kuliko kazi" amesema.






## Magufuli awapaisha Stamina, Profesa Jay

NI wazi Rais Magufuli, amewapeleka mbali wasanii Stamina na Profesa Jay, baada ya wimbo wao 'Baba' kutazamwa na idadi kubwa ya watu kwa siku chache.

Juzi akiwa katika uzinduzi wa Jengo la Jitegemee na Studio za Channel Ten Plus, Radio Magic FM na Radio Classic FM, Rais Magufuli, aliomba wimbo huo kuchezwa kama kibao chake bora kwa mwaka 2021.

Baada ya tukio hilo, idadi ya watu waliotazama kupitia mtandao wa You Tube, ilipanda kwa kazi na kufikia zaidi ya milioni 1.8.

Kupitia ukurasa wa Instagram wa Stamina, amemshukuru Rais kwa kuandika

"Sijui nilie, sijui nicheke, yaani sielewi aiseh kwa furaha niliyonayo,sina neno lingine zaidi ya Asante kwa Rais wangu Magufuli, kikubwa uhai...asante Mungu."

## Hiyari Yangu; Ngoma si yako, kibwaya cha nini?

**Na Adam Fungamwango**

FILAMU hii iitwayo 'Hiyari Yangu', imechezwa na wasanii Simon Mwapagata, Suleiman Barafu, Wellu Sengo, Muhogo Mchungu na wengineo.

Mwapagata na mkewe Wellu wanaonekana kuishi maisha ambayo ni tofauti na ilivyozoeleka kwa jamii yetu ya Kiafrika baina ya mume na mke.

Mume anapika chakula, anafua nguo na kufanya kazi zote za ndani, huku mkewe akiwa ametulia tuli.

Hali hiyo inamkera mno kaka wa Mwapagata, aitwaye Barafu aliyekuja kuwatembeea, na anamkanya ndugu yake asiwe bwege. Hata hivyo yote hayo hayakusaidia, jamaa aliendelea na kazi zote za nyumbani, huku mke akiwa na kazi ya kupeleka watoto shule na kuwarudisha, lakini anaporejea anatulia tu nyumbani huku akichati na simu.

Hali ilipozidi kuwa mbaya, Barafu akaamua kuondoka nyumbani kwa mdogo wake kwani hakuweza kuvumilia hali ile. Akakimbilia kwa baba yake mdogo, Muhogo Mchungu na kumueleza kuwa mdogo wake amepewa limbwata na mkewe, kwani imefikia wakati sasa anakuna hadi nazi, mkewe akiwa amekaa tu.

Muhogo anaamua kufunga safari hadi kwa mtoto wa ndugu yake na kukuta yale yale aliyosimuliwa.

Pamoja na kumuweka chini mkewe akiwa hayupo, lakini Mwapagata hakusikia, aliendelea na kazi zake kama mtoto wa kike.

Alipoondoka wenyewe walicheka na kukumbushana kuwa bado siku tatu tu.


Wellu, mke wa Mwapagata anaitisha kikao cha wanandugu wote, lakini wa kiume baadhi walisusa, kutokana na walichokiona. Kwenye kikao hicho Wellu alifafanua kuwa mumewe aliamua kufanya kazi zile kwa hiari yake kwa muda wa mwezi mmoja ambao yuko likizo ili kuangalia uzito na kazi za akinamama.

Akasema walikuwa wanabishana na mumewe kwa kuwa kuna wakati mke analalamika kuwa anachoka, hivyo akasema atakapopata likizo atakuwa akifanya kazi zote za ndani ili aone kama zinachokesha kweli au la.

Mwapagata alikiri hilo na kusema kuwa kesho akaanza kazi ofisini na kazi za ndani zitaendelea kwa mkewe kama kawaida na hali ile haikuwa kama wengi walivyotafsiri kuwa amelishwa limbwata. Wengi walishangaa na wambea wakabaki midomo wazi. Vizabizabina na visalata wa mtaa likawashuka.





## Wastara akumbuka ndoa ndoano

MWIGIZAJI mkongwe wa filamu nchini, Wastara Juma, ametoboa siri ya kuvunjika kwa ndoa yake ya pili, akisema dalili ya kupewa talaka ilianza kutawala siku 10 baada ya kuolewa.

Ndoa kati ya Wastara na Mbunge wa Jimbo la Donge Zanzibar, Sadifa Juma, ilivunjika siku chache na kuibua mjadala mkali kwa watu huku wakimalumu msanii huyo kuwa chanzo cha kuondoka mapema katika ndoa yake.

"Nimeolewa sio kwamba nilikuwa napenda ila mwisho wa siku mimi ni muislam na sitaki kuzini, hakuna atakayeniongelea vizuri labda marehemu Sajuki kama angekuwa hai ndio angeweza kunielezea Wastara ni mwanamke wa aina gani" amesema Wastara wakati akizungumza katika kipindi cha Mama mia kinachorushwa na East Africa Radio

"Kabla sijaingia kwenye ndoa mume wangu alikuwa anatuma vizuri, ananitumia kama laki tatu au mbili baada ya kuingia kwenye ndoa ilikuwa mtihani kweli,

kwanza ndoa ilikuwa inasitasita, nilikuwa nikiongelea naye kidogo nasikia anasema basi nikupe talaka, na hilo neno nilianza kulisikia siku kumi baada ya kuolewa" ameongeza.

## 5 bora za Waziri Sonyo

**Na Adam Fungamwango**



JUMANNE iliyopita, tasnia ya muziki wa dansi ilipatwa na mshituko baada ya taarifa za kifo cha mwimbaji mwenye sauti nyororo, Waziri Sonyo.

Mwanamuziki huyo aliyezipigia bendi ya Mviko Sound, Chuchu Sound, TOT Plus, African Revolution 'Tamtam', Double M na nyingine nyingi.

Kwa mujibu wa ndugu wa marehemu ni kwamba, Sonyo alifariki dunia kutokana na ugonjwa wa moyo, muda mfupi tu baada ya kutoka kuangalia mechi kati ya Simba dhidi ya Al Ahly.

"Nilizungumza naye kipindi cha mpumziko cha mechi, lakini alipofika nyumbani, akiwa mlangoni tu alijisikia vibaya na kuanguka chini. Niliwaomba wadogo zangu wampatie dawa alizokuwa akizitumia, lakini hakuweza zilipoletwa kwani tayari alikuwa ameshafikwa na umauti," alisema Saniti Sonyo mmoja wa ndugu wa marehemu.

Amefariki Kibaha mkoani Pwani na kuzikwa huko huko akiwa na miaka 44, akiwa mmoja wa wanamuziki wa kizazi kilicholeta mabadiliko miaka mwanzoni mwa 2000, ikiwa ni athari wa ujio wa bendi ya Wenge Musica nchini mwishoni mwa miaka ya '1990.

Ziafuatazo ni nyimbo kali ambazo Sonyo aliziimba akiwa na bendi mbalimbali na kumpatia sifa kubwa.

**Usione Vyaelea-Chuchu Sound**

Akiwa kwenye bendi ya Chuchu Sound, mwanamuziki huyo aliimba nyimbo mbalimbali ikiwamo 'Usione Vyaelea'. Kwenye wimbo huo kuna sauti yake akiimba 'Kila ukionacho wakata kiwe chako, kila usikiacho wataka kukiona kwa macho.'

Ni moja kati ya nyimbo zilizoanza kuwafanya mashabiki wa muziki kuanza kumfuatilia na kukishangaa kipaji hicho kipya cha muziki, mwanzoni mwa miaka ya 2000.

**Masimango-TOT Plus**

Huu ni wimbo wake maarufu zaidi kuliko zote alizowahi kutunga na kuimba. 'Masingango' ni wimbo uliotokea kupendwa na kuwa tishio akiwa TOT Plus na hapo ndipo kila mmoja akamjua Sonyo.

"Kwa kuwa vimekuwa dhahiri machoni mwangu, maji ya shingo yamenifika nashindwa kuvumia, ni bora kwetu kule alikobaki kaka..." Ni moja kati ya maneno aliyoyaimba kwenye wimbo huo bora kabisa.

**Sweet Baby-TOT Plus**

Ni mmoja ya nyimbo safi ambazo ziliimbwa kwenye mtindo wa mduara hivi. Kipo kipande cha Sonyo ambacho aliimba 'Tulikuwa sote tulipata tabu, hatukujali maneno ya watu.'

Ni moja kati ya nyimbo zilizozidi kumpaisha Sonyo. 'Ilove Sweet Baby, nakupenda kwa dhati Sweet Baby, tumevumilia mengi Sweet Baba, sasa tuko fresh tunavinjari.' Hicho ni kiitikio cha ngoma hiyo.

**Mengi Yamenikuta-Tamtam**

Akiwa na African Revolution waka 'tamtam', Sonyo alitunga na kuimba kibao kimoja kiitwacho 'Mengi Yamenikuta.'

Katika wimbo huo anasema yaliyomkuta ndiyo ya kidunia, kwani hata Yesu, pamoja na mafundisho yake mazuri, lakini Wayahudi walimkamata, kumpiga na kumtesa, sembuse yeye hatoshangaa.

**Ndoto-Jiti**

Wimbo huu ulipigwa kwenye mahadhi ya muziki wa kisasa. Alishirikishwa na msanii aitwaye Jiti.

Ni msanii aliyekuwa akiimba nyimbo za Hip Hop, hivyo akamshirikisha Sonyo ili kuweka ladha ya sauti yake mwembamba na kuimba, ili mashabiki wapate ladha mbili kwa wakati mmoja, kufokafoka na kuimba.



# Kim kweli humtaki Kanye West?

MWANAMITINDO na mshiriki wa kipindi cha maisha halisi katika televisheni, Kim Kardashian, amekamilisha kufungua kesi ya madai ya talaka dhidi ya mume wake Kanye West.

Kulingana na mtandao wa TMZ, katika madai hayo Kim anataka kuhakikishiwa kisheria juu ya mgawanyo wa mali na matunzo ya watoto wao wanne aliozaa na mwanamuziki huyo.

Hata hivyo, hakuna utata wa mali waliozochuma wakati wakiwa wanandoa, kwani Kim na Kanye wamefanya makubaliano ya kisheria kama kutatokea wataachana.



## Bobby karibu tena uraiani

MWANAMUZIKI wa Hip hop wa Marekani, Ackquille Jean Pollard. Maarufu kama Bobby Shmurda, hatimaye amekuwa huru baada ya kutoka gerezani kwa msamaha.

Kulingana na mtandao wa TMZ, rapa huyo aliachiliwa kutoka katika gereza la Clinton Correctional Facility lilopo katika jiji la New York siku ya Jumanne ya wiki hii.

Kutoka gerezani kwa msanii huyo kunatokana na kupata msamaha wa parole ambao ulimfupishia kifungo chake cha miaka mitano alitakiwa kukamilisha Feb 13 mwaka 2026.


## Kumbe Joeboy analelewa na jimama

MWANAMUZIKI kutoka Nigeria, Joseph Akinwale Akinfenwa, ambaye anajulikana kama Joeboy, ameibua mjadala mkali baada ya kukiri anashiriki mapenzi na mwanamke aliyemzidi umri.

Akifanya mahojiano na redio moja nchini humo, Joeboy, amesema analelewa na mama huyo ambaye amekataa kumtaja jina.

"Bado sijaoa, lakini nina marafiki wengi wa kike, bado nalelewa na mwanamke mmoja siwezi kusema jina lake , ukweli nina sugar mama," amesema.





## Vector unawachokoza wanaharakati

RAPA wa Nigeria, Vector, ametoa ushauri kwa wanawake kujilinda wao wenyewe kwa wanaume wanaotaka kuwanyanyasa kijinsia.

Akiandika katika ukurasa wake wa Twitter, staa huyo wa muziki amewashauri wanawake ambao hawana wanaume ambao wanapata muda wa kutoka sehemu mbalimbali kujilinda wenyewe pale inapowatokea matatizo.

"Wapenda wanawake wanaishi peke yao, endapo anatokea mwanaume anataka kukushika, chukua silaha kabiliana naye," amesema.

## Uju hongera yako kumiliki ndinga kali

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Uju Okoli, amezidi kujipambanua kuwa yupo juu baada ya kununua gari jipya la kifahari aina ya Lexus.

Baadhi ya mastaa walimpongeza kwa hatua yake hiyo, huku Georgina Ibeh, alishiriki picha ya staa huyo akiwa katika gari lake kwa kuandika ujumbe wa kumtakia kila la kheri.

Ingawa Okoli hakuweka picha hiyo katika mtandao wake, Ibeh, ndiye aliyeiweka katika akaunti yake ya Instagram na kuibua maoni tofauti kwa mashabiki wake.



MAKALA

# Uhifadhi malikale unaposigana na desturi, tamaduni za pwani

**Na Michael Eneza**

KUNA mwamko miongoni mwa wadau wa hifadhi za taifa na hasa jinsi unavyohusiana na utalii, hasa raslimali hai katika mbuga za wanyama na malikale zinazomilikiwa na Makumbusho ya Taifa.

Kinachounganisha na kutatiza hisia hizi hasa ni malikale za maeneo ya pwani, ambazo kwa sehemu kubwa ziko Unguja, eneo la Mjimkongwe, na kwingineko kama Kilwa, Bagamoyo, Pangani, Mtwara na maeneo kadhaa mengine.

Wadau wa uhifadhi na wanataaluma wanajiuliza kama suala ni hifadhi ya majengo ya kale au ni pamoja na utamaduni wa jadi, ambao upo.

Taswira ya mjadala huo ilijitokeza bayana hivi karibuni katika majadiliano na mdau hifadhi akielezea mwelekeo wa kimkakati wa Makumbusho ya Taifa, ambayo iligusa kwa karibu mjadala wa ziada kuhusu maendeleo ndani ya mwelekeo wa hifadhi.



Moja ya magofu yanayopatikana mji wa kale wa Kilwa Kisiwani

Alielezea dhana ya kisasa ya hifadhi na makumbusho kwa upana usio wa kawaida, akijibu swali au mtazamo wa mwendesha kipindi kuwa mtu akipita maeneo ya pwani (yenye malikale nyingi zaidi hapa nchini) kuna mdororo wa maendeleo. Kuna aina ya utulivu na kukosa uharaka, wepesi wa kubadili kilichopo, majengo ni yale yale, watu ni watulivu na hawahangaiki.

Mwendesha kipindi cha redio alieleza hali hiyo kwa hisia, akitaka kuwe na maendeleo katika maeneo hayo, wakati mdau hifadhi alikuwa na mwelekeo wa mawazo au mtazamo tofauti kabisa. Kwa mwelekeo wa hisia zake, kinachohifadhiwa katika maeneo ya malikale kama ya pwani siyo majengo chakavu tu ila mifumo ya jamii na tamaduni zake.

Kwa maana hiyo mazingira ya kutokuwa na haraka, kuwa na utulivu, kutobadilika mandhari ya miji hiyo na mwendelezo wa utamaduni wake kwa jumla ni sehemu mahsusi siyo kwa maana ya kitu kilichopita, ila hifadhi ya utamaduni.

Ndiyo hapo unakuja mgongano kati ya maendeleo na viashiria au vielelezo vyake ambavyo alikuwa anaulizia mwendesha kipindi, kuwa ni haba kuviona maeneo ya pwani hasa haya yenye malikale za hifadhi.

Mdau wa hifadhi akaonyesha kuwa hali hiyo si tatizo ila ni aina ya ushindi na pia ni jambo la kujivunia kuwa tumehifadhi utamaduni wetu, haujaharibiwa na wageni, na watu wanakaa mithili ya jinsi walivyoishi wakati malikale hizo zinajengwa, kuwa majengo yanachakaa ila jamii zinadumu, hazichakai.

Licha ya kuwa unaweza kuweka mezani mjadala wa jema au baya, kutunza tamaduni za jamii tofauti nchini bila kubadili chochote, au kuweka nakshi hafifu hapa na pale. Mifano halisi ni kila mtu kuwa na ndala badala ya kutembea peku, au nyumba kupigwa bati, chokaa na 'ripu' badala ya udongo, mabati mekundu na hata kusakafia kwakiwango fulani badala ya udongo, nyasi, vumbi na funza.



Moja ya mtaa wa Kilwa Kivinje.

Si rahisi kusema kuwa aliyetaka hifadhi ya utamaduni wa watu wa pwani anaashiria ulivyo sasa pamoja na hayo mabadiliko ya taswira yake ya nje, au angekuwa tayari kuona zikiwa katika uduni wake asilia, wa vumbi.

Mkakati wa kupanua shughuli za Makumbusho ya Taifa ukitafsiriwa kuwa ni pamoja na kutunza mifumo ya jamii husika na hulka zao kwa jumla ni hisia ya kimapinduzi kwa wanaharakati, hasa walio mstari wa mbele wa lugha ya Kiswahili.

Ni mvutano ambao umekuwa katika mifumo ya elimu na tafsiri ya kupigania uhuru au kutaka maendeleo, kuwa vianzio vya dhana hizo vinakinzana, ambako mabadiliko au maendeleo yanapangua mifumo ya jadi.

Dhana za kizalendo na kiharakati zinaitetea mifumo ya jadi kuwa inafaa, siyo ya kigeni.

Baadhi ya wanaharakati kwa mfano walipinga kwa nguvu kuvunjwa kwa nyumba za jadi za vyumba sita mtaa wa Kariakoo jijini Dar es Salaam, na badala yake kujengwa nyumba za wastani wa ghorofa sita.

Ni mandhari yanayopendezesha jiji na kuongeza idadi ya waajiriwa katikati ya jiji. Ndiyo hasa maendeleo.

Upo mfano uliotolewa na mdau wa hifadhi na upana wa dhana ya makumbusho ya taifa uliokuwa wa aina yake katika kutoa picha halisi ya tamaduni hizi, na kuyakinisha kwa wenye mashaka na lengo la hifadhi yake.

Alisema katika kutetea dhana ya utulivu wa jamii za pwani, kufanya mambo yao kwa utaratibu bila haraka, kuwa 'mtu anaweka begi lake barabarani anaingia ndani, basi likifika linapiga honi, anakuja anachukua begi lake anapanda.'

Ina maana kuwa hakuna uwezekano wa wizi mahali hapo, hali ambayo inafahamika pia kwa upande wa Zanzibar; kuna wakati vitu vilivyopotea vinatangazwa redioni, mwenyewe anatafutwa afike kituoni achukue mali iliyoonekana. Inaonekana ndiyo ustaarabu kukamilika.

Picha hii inaweza kurudiwa kwa njia tofauti kwa jamii takriban zote nchini ambako maisha ya kisasa bado hayajaingia kwa kina, ingawa kimsingi jamii kama hizo zinazidi kupungua kila iitwapo leo.

Kwa wanaharakati wa utamaduni inaonekana kuwa ni tabia njema za wakazi wa pwani, malezi mazuri ya wazazi kwa watoto wao na ushauri kwa vijana, n.k.

Hali halisi ni kuwa na jamii iliyojifunga kiimani na kihisia, ukipita mstari tofauti na huu unaondolewa kwa njia moja au nyingine, alichowahi kusema Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Mwinyi kuhusu kipindi chake cha ubunge wa Mkuranga.

Alisema waliona wenyeji wa hawawezi kujenga nyumba za bati, kwani atakayeanza au waliowahi kuanza yaliwafika, wakatafakari hali hiyo wakagundua kiini chake kisaikolojia.

Inafanya kazi ndani ya watu wa jamii ile, wazawa, na haihusiki na wageni wakifanya hivyo.

Kwa njia hiyo uongozi wa wilaya ukaanza kukaribisha wageni hasa kutoka mkoani Kilimanjaro kufungua biashara, pakaanza kuchangamka na wengine wakaanza 'kudandia' ambao mwanzoni wasingethubutu.



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Doroth Gwajima, akielezea tiba asili ya magonjwa ya upumuaji.

# Ndivyo Tanzania inavyohitaji msukumo mpya wa tiba asilia

Na Christina Mwakangale

TIBA asili kwa nchi za Afrika zimeanza kutumika tangu enzi, ingawa hazijafanyiwa utafiti na kupewa msisitizo kama ilivyo kwa mataifa ya India na China.

Sababu mbalimbali husababisha matumizi hayo kuwa duni ikiwamo upatikanaji, utafiti na kuziboresha, vipimo na dozi, mfumo wa uzalishaji na ufungashaji.

Mtaalamu wa Mimea kutoka Shirika la Dawa Asili na Ulinzi wa Mazingira (TRAMEPRO), Dk. Isaac Mittoh, anaiambia Nipashe kuwa, Tanzania ikijikita katika kuzalisha tiba ya asili itokanayo na mimea au wanyama itaongeza pato la taifa.

Anasema tiba asili ambayo inahusisha maarifa ikiwamo utafiti, na ikitumika ipasavyo ni kinga kwa binadamu katika magonjwa mbalimbali kama vile saratani na kisukari.

"Kuna ambao huzaliwa na magonjwa yasiyoambukiza, tiba asili afya bora na humsaidia binadamu katika magonjwa, ina kinga kuzuia kupata magonjwa yasiyoambukiza kama saratani na kisukari."

Wapo wanaozaliwa na udhaifu fulani lakini utaratibu wa kutumia mimea kwa asilimia 80 ukawa umepunguza uwezekano wa kupata magonjwa hayo, anasema Dk. Mittoh.

Pia anasema tiba asili inahitajika sasa kujaribu kupambana na magonjwa sugu ikiwamo saratani. "Unafanyika utafiti sasa kwa takribani miaka 200 kuhusu saratani sasa na inatafutwa dawa bila mafanikio duniani. Tiba asili ikiendelea kuboreshwa ikawa nzuri, mfano si kupewa magome ya mti au dawa ambayo ni chungu inaweza kuwekwa kwenye mfumo wa 'syrup' (dawa ya maji) ikapunguzwa uchungu," anasema Dk. Mittoh.

"Wakati Shirika la Afya Duniani (WHO) likisema bangi au marijuana zilizo katika aina kuu mbili ni dawa ambayo mtu akiitumia inamletea 'reaction' na utaratibu wa mwili mzima unabadilika na inakuwa kama kilevi ni kutokana na kutumika bila maelekezo."

Mittoh anasema mmea huu unatumika kusaidia walio na matatizo ya kusahau kwa aina ambayo ikitumika kwa usahihi na kuondoa viambata ambavyo havitakiwi," anasema.

Anabainisha kuwa Tanzania inaweza kuingia katika soko la dunia kutokana na kukua kwa mahitaji ya tiba asili na kwamba hadi kufikia mwaka 2026 uuzaji wa dawa za asili duniani utakuwa na thamani ya Dola bilioni 411.

"Tanzania tutakuwa wapi katika kuchangia katika soko la dunia? Wizara ya Afya ikiwa msimamizi inaweza kusimamia mashamba kwa ajili ya kuzalisha mimea mbalimbali ili kupata dawa," anasema Mittoh.

Anasema kuwa utafiti wa mimea na wanyama kwa ajili ya tiba asili inayoweza kutibu magonjwa ikagundulika na kupitishwa na mamlaka zenye wajibu wa kuhakiki viwango itasaidia kuimarisha biashara ndani na nje ya nchi," anasema Dk. Mittoh na kuongeza...

"Tiba asili inahusisha maarifa, mimea kama taifa tukiweza kuendeleza katika uzalishaji wa dawa hizo na kuzifungasha kisasa, tutaifanya Tanzania kuingia katika soko la dunia ambalo linahitaji tiba hiyo kwa kiwango kikubwa hivi sasa."

Mittoh anasema tiba asili ikiendelezwa kwa kuwapatia watu elimu itaondoa dhana kuwa ni uchawi na kwamba uelewa kwa jamii kuhusu tiba hiyo itakuza matumizi.

Vilevile, Dk. Mittoh anasema sekta ya utalii na kilimo zinaweza kukua kwa kuleta watalii na kwenye kilimo na mtu moja mmoja anaweza kuwekeza katika klimo cha mimea tiba.

Mpaka sasa naweza kusema kwamba Tanzania kuna dawa ya mitishamba muhimu ambayo ina uwezo wa kutoa tiba kwa kutumia maarifa na kusaidia mtu kwa asilimia 90 hadi 100 kwa wenye saratani bila kujali yupo katika hatua ya nne, tatu, pili au kwanza ya ugonjwa huo," anasema Dk. Mittoh.

"Tukiwa na mashamba tukawekeza kwenye maarifa, ya uzalishaji tutaona mataifa ya nje yakija nchini kutaka kujua tiba inafanyikage na ufanisi wa dawa," anasema.

Mittoh anafafanua kuwa inahitajika ufungashaji bora wa dawa za tiba asili katika mfumo tofauti ikiwamo zilizosagwa na kuwa unga, vidonge au maji, za kupulizia na za kupaka.

Pia anasema kukua kwa teknolojia kunaifanya tiba hiyo kuondoka katika mfumo wa magome ya miti ambayo haukuzingatia usafi.

"Hivi sasa kuna magonjwa au vimelea vingi zinahitajika juhudi zaidi kuongeza ubunifu katika kufungasha na kumpatia mtu dawa hizi katika kifungashio bora," anasema Dk. Mittoh.

Anasema kwa nchi zilizoendelea utafiti ulianza mapema katika namna ya kuboresha tiba asili na kuitumia kirahisi na kikamilifu.

**MAFUNZO**

Dk. Mittoh anasema Tanzania inaendelea kurasimisha tiba asili kwa kufuata mwongozo wa Shirika la Afya Duniani (WHO), katika Azimio la Mwaka 1978.

"Kwa Tanzania kupitia azimio hilo, WHO ilisema watu wanaotumia tiba asili kila nchi waiendeleze na ipatikane kwa urahisi na kumfikia mtumiaji bila vikwazo," anasema.

Hapa nchini, Dk. Mitoh anasema kuanzia 2013 yalianza kutolewa mafunzo ya kozi fupi kutoka katika taasisi na vyuo vya afya ikiwamo Muhimbili kuhusu tiba hizo.

"Mafunzo ya namna ya kumhudumia mgonjwa, kupakia dawa katika vifungashio, mfumo wa vidonge na iwapo mgonjwa amefikia hatua fulani umsaidie apate huduma ya haraka na akiwa hatua hii apelekwe hospitali," anasema.

Anasema Chuo cha Kilimo Sokoine (SUA), kinatoa mafunzo kama hayo kwa kutumia mimea na kwamba mkakati ni kufikia mafunzo ya ngazi ya shahada kwenye eneo la tiba asili.

HABARI KIMATAIFA

# Joe Biden ateta na Kenyatta

**Nairobi, KENYA**

RAIS wa Marekani, Joe Biden amezungumza na Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya,kuhusu suala la mgogoro Tigray.

Mazungumzo hayo yamefanyika kwa njia ya simu juzi, Ikulu ya White House ilisema.

Viongozi hao wawili walijadili kuzorota kwa haki za binadamu na hali ya kibinadamu jimboni Tigray, nchini Ethiopia.

Walizungumza kuhusu hitaji la kuzuia vifo na kuhakikisha misaada ya kibinadamu inawafikia.

Tigray imekumbwa na mzozo tangu Novemba kati ya vikosi vya Ethiopia na vikosi washirika wa Chama cha Tigray People's Liberation Front (TPLF).

Maelfu ya watu wanaripotiwa kuuawa, na karibu milioni mbili wamekimbia makazi yao.

Shirika la Msalaba Mwekundu mwaka huu, limeonya kuwa uhitaji wa msaada wa kibinadamu ni mkubwa mno.


Ikulu ya White House ilisema kuwa Rais Biden alisisitiza kujitoa kwake kufanya kazi na Kenya kusaidia uimarishaji wa amani na usalama katika eneo hilo.

Katika hatua nyingine, ripoti mpya ya Shirika la Kimataifa la Amnesty inaonyesha kuwa wanajeshi wa Eritrea wametekeleza mauaji ya watu katika jimbo hilo.

Ofisa wa Amnesty, Deprose Muchena, alisema kilichotekelezwa na wanajeshi hao na wale wa Ethiopia ni uhalifu wa kivita.

Ethiopia imekuwa ikikanusha kuwa iliwatumia wanajeshi wa Eritrea katika operesheni hiyo.

**BBC/UN**



Picha iliyotumwa duniani na chombo kilichopewa jina la Perseverance rover kinachochunguza sayari ya Mars siku tatu baada ya kutua salama Februari 18, mwaka huu. **(PICHA: AFP)**

# S. Kusini kutoa chanjo watoto milioni 2.8

**Juba, SUDAN KUSINI**

SUDAN Kusini kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) na Shirika la Afya Duniani (WHO), juzi wameanza kutoa chanjo ya polio kwa watoto milioni 2.8.

Awamu ya kwanza ya chanjo ilifanyika Novemba na Desemba mwaka jana na kuwafikia watoto milioni 2.6.

Mkurugenzi Mkuu wa Afya ya Msingi wa Wizara ya Afya ya Sudan Kusini, Atem Nathan, alisema mlipuko wa polio ulitangazwa Septemba 18, mwaka jana na sasa umeenea kwenye kaunti 17 za nchi hiyo.

Majimbo ya Warrap na Bahr El Ghazal Magharibi ndio yaliathiriwa zaidi.

Mwakilishi wa WHO nchini Sudan Kusini, Olushayo Olu, alisema ili kuzuia ugonjwa huo, wadau wameimarisha ufuatiliaji na kuweka mkazo kwa jamii na vituo vya afya kufuatilia watoto ambao wamepooza miguu ghafla.

Alisema kampeni ya sasa inalenga kutoa fursa kwa watoto walio kwenye hatari kupata uingiliaji wa haraka unaoweza kuepusha vifo na ulemavu kutokana na ugonjwa huo.

Nathan alisema kwa msaada wa mpango wa kimataifa wa kutokomeza polio, GPEI, serikali inaendesha awamu ya pili ya kutoa chanjo dhidi ya aina hiyo ya polio (mOPV2).

"Siyo tu kwa ajili ya kukabili mlipuko bali pia kuhakikisha Sudan Kusini inakuwa haina polio kabisa na wakati huo huo kuimarisha huduma za kila wakati za utoaji wa chanjo."

Alitoa wito kwa wazazi na walezi kuruhusu watoto wao kupatiwa chanjo na wahudumu wa afya wanaopita nyumba kwa nyumba.

Dk. Olu alisema kampeni ya sasa inatoa fursa kwa watoto walio hatarini zaidi kupata hatua ya kina inayoweza kuepusha magonjwa yanayotishia maisha ikiwamo polio ambao husababisha ulemavu wa maisha.

**CRI**

# Mamia ya wanafunzi wa kike watekwa Nigeria

**Lagos, NIGERIA**

MAMIA ya wanafunzi wa kike wametekwa nyara, Kaskazini Magharibi mwa Jimbo la Zamfara.

Shirika la Habari la BBC, lilipewa taarifa ya tukio hilo.

Mwalimu wa shule, alisema takribani wanafunzi 300 wametekwa, jana.

Msemaji wa serikali, alisema eneo hilo limethitishwa kutokea kwa shambulizi majira ya asubuhi, bila kutoa maelezo ya kina.

Idadi hiyo ni kubwa ikilenga kuteka wanafunzi shuleni kwa wiki za hivi karibuni huku watu wenye silaha wakiwateka watoto wa shule.

**REUTERS**

# Japan yamteua 'Waziri wa Upweke'

**Tokyo, JAPAN**

WAZIRI Mkuu, Yoshihide Suga, amteua Tetsushi Sakamoto kuwa Waziri wa Upweke nchini Japan.

Kutokana na ongezeko la visa vya kujitoa uhai miongoni mwa umma wa Japan na sababu ya janga la corona (Covid-19), Waziri Mkuu Suga alimteua Tetsushi Sakamoto kushika wizara hiyo.

Katika mapambano dhidi ya virusi vya corona, maisha ya jamii yalisimama na kuufanya umma kuzidi kupata shinikizo la kimawazo na upweke.

Kumekuwa na ongezeko la visa vya kujiua nchini humo.

Ili kuchukua hatua za kuzuia kuongezeka kwa visa vya kujitoa uhai, Waziri Mkuu wa Japan, Suga alimteua Waziri wa Maendeleo ya Mkoa, Sakamoto kuwa kama waziri anayehusika na shida za watu wanaoishi na upweke.

Sakamoto, katika taarifa yake ya kwanza aliyotoa baada ya uteuzi mpya alisema:

"Waziri Mkuu Suga ameniamuru kuchunguza suala hili na kuweka mkakati kamili wa uratibu na wizara husika.

Natumai tutafanikisha kufanya shughuli za kuzuia kutengwa kwa jamii na kuulinda uhusiano kati ya watu.

**TRT**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

***Uza,***
***Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***
***Tupigie 0782253676***

## KUPOTEA KWA CHETI



**Eliaichi Menye Manga** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index number **SO800/0515** kilichotolewa na Loyola High School mwaka **2016.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/MAG/RB/70595/2021.**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO...... 2020**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE YOHANA MABENE CHAWALA**

**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY ANDREA YOHANA CHAWALA**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before 11 day of 3 2021.
Dated at Dodoma this 27th day of January 2021.
**Presented for filling this 24 day of 2 2021.**

MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA DISTRICT

---

**MWAMBA AUCTION MART AND RECOVERIES**
P.O.BOX 429 DODOMA – TANZANIA
OFFICE LOCATION: CCM REGIONAL BUILDING ROOM No. 9
0715170553 / 0756011439

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa Amri ya Mahakama ya Mwanzo Chamwino Mjini, wilaya ya Dodoma nitauza mali ya SAMSON MKOPI ambayo ni Nyumba zilizo kwenye Kiwanja chenye vipimo **(806875,9315734), (806859,9315733), (806872, 9315757), (806866, 9315765)** makulu jiji la Dodoma ili kufidia deni analodaiwa na **SIMON NGATUNGA**. Mnada utafanyika Nyumba zilipo na zitauzwa kama zilivyo siku ya tarehe **12/03/2021 Saa Nne 10:30 asubuhi.**

**MASHARTI YA MNADA KISHERIA**

- Mnunuzi atalipa asilimia 25 (25%) ya bei papo hapo na asilimia 75 (75%) atailipa ndani ya siku 14.
- Mnunuzi akishindwa kulipa asilimia 75 ndani ya siku 14, mnada utarudiwa na asilimia 25 haitarudishwa
- Mnunuzi akishanunua gharama za kubadili umiliki ni juu yake.

**MAWASILIANO simu namba**
**(+255)735/715) 170 553 COURT BROKER.**

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi**
**NO.53/2021**

**Ombi la BERNADETHA CYPRIAN CHIMAZI kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu EVARIST ANDREA MODEST**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 29/03/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 25/02/2021**

Tarehe 25/2/2021
Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FARIDA MOHAMED HASSAN** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA RAV 4** yenye namba za usajili **T 542 BBT** chasisi namba **JTEHH20V800081117**,yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **DAR/BUG/RB/109663/2021**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

**HADITHI**

# HADITHI


MAUAJI ya kutisha yanatokea ndani ya gesti moja maeneo ya Kigogo jijini Dar es Salaam. Mfanyabiashara Burhan anauawa ndani ya gesti ya Tukutane, akiwa na msichana mmoja mrembo aitwaye Mwanaidi. Polisi wanawakamata watu wote waliokutwa humo, pamoja na wafanyakazi wa gesti hiyo kwa ajili ya mahojiano. Lakini inaonekana muda ambao walikuwapo wapenzi hao hakukuwa na mteja mwingine yeyote zaidi yao.

Baada ya mahojiano ya kina, inaonekana kabisa kuwa Mwanaidi ndiyo muuaji. Je, ni kweli? Kwa nini alimuua mpenzi wake wakiwa wamejifungia chumbani? Fuatilia hadithi hii kwa makini ambayo mbali na kukutia simanzi, furaha na kukuburudisha, pia itakufundisha, elimu na kufunulia mambo ambayo hukupata kuyafikiria kabla.

# Lazima Apatikane - 10

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**




"Sikiliza Mwanaidi, una kesi mbili sasa za mauaji. Ya kwanza ni kumuua mpenzi wako Burhan, ya pili ni kumuua Tiika, mfanyakazi wa benki. Sasa mimi nimeona nikusaidia kitu kimoja tu. Nikutandike risasi ya kichwa ili uzikwepe kesi hizi zote mbili. Kumbuka kesi moja tu inatosha kabisa kukutia kitanzi."

Ghafla ujasiri wa ajabu ukamjia Mwanaidi, akajikuta maneno yakimtoka kinywani.

"Naomba unisamehe Martin. We uniache tu mimi na kesi zangu. Hata kama nitanyongwa huko mbele ya safari sawa tu, lakini kwa sasa naomba unisameke."

"Nikusamehe ukawaambie polisi kuwa nimekutuma kwenda kumuua Tika?"

"Siwaambii?"

"Hata kama hukuwaambia. Watafanya uchunguzi na watakubaini na wewe utawaambia kuwa ni mimi. Ili mimi niwe salama ni lazima wewe ufe. Hata kama wakijua ni wewe tayari utakuwa umeshakuwa marehemu, hivyo uchunguzi utaishia hapo. Watajua kuwa aliyemuua Tika ni Mwanaidi. Mwanaidi yule yule aliyemuua mpenzi wake Burhan, kwisha."

Machozi yalimtoka Mwanaidi. Hakuwa na tumaini lolote sasa la kubaki hai. Kuna wakati aliona ni bora risasi ipenye kwenye kichwa chake ili akapumzike kutokana na kesi mbili za mauaji, moja imeshaanza kumkabili na nyingine itamkabili baadaye. Lakini siku zote kifo hakizoeleki, woga wa kufa unamwingia na kuona ni bora aendelee kuwa hai ili apambane na kesi hizo.

Hata hivyo akiiangalia sura ya Martin hakuona dalili yoyote ya yeye kubaki hai. Aliongea maneno ambayo hayakutoka mdomoni. Ndiyo kwa mara ya kwanza akaanza kujuta kukutana na Burhan.

Ni Burhan tu ndiye aliyemletea matatizo yote haya. Pamoja na kumpenda na pesa nyingi alizompa, lakini kazi yake ya ujambazi ndiyo imemletea kupata kesi zote mbili za mauaji.

"Mimi nadhani nisipoteze muda Mwanaidi. Sikupenda kukuua mtoto mzuri kama wewe. Lakini nimelazimika kufanya hivyo. Kwa heri. Nenda kamsalimie Burhan mpenzi wako mwenyewe ambaye ukaamua kumuua kwa ajili ya zile milioni mia moja zilizokuwa kwenye mfuko wake." Alisema huku mkono wake ukinyooka kutaka kumfyatulia risasi Mwanaidi.

"Ngoja kwanza Martin, samahani naomba usiniue kwanza." Alilia Mwanaidi.

"Muda umekwenda sana, unataka nikeshe hapa tunabembelezana?"

"Nakufa hapa, lakini nataka kumwambia jambo moja tu ambalo utawaambia walimwengu."

"Lipi."

"Sijamuua Burhan. Naona wewe umekuwa unanihukumu hapa kabla sijafa, niue lakini Burhan mwenyewe huko mbinguni ninakokwenda anajua ukweli."

Maneno hayo ya Mwanaidi yalifuatiwa na kicheko kikali cha kebehi, kilichochanganyikana na dharau.

"Kwa sababu umeyataka mwenyewe, ngoja nikwambi kitu." Alitamka Martin baada ya kumaliza kicheko chake.

"Sikuwa na nia ya kutaka kumwambia. Nilitaka ufe ukajue mbele ya safari. Kwa sababu umetaka. Ngoja nikwambie. Mimi ndiye niliyemuua mpenzi wako Burhan." Alisema kwa namna ya majisifu na kumfanya Mwanaidi ashikwe na mshangao. Ni kama vile alisahau kidogo kama kifo chake kipo mlangoni.

"Heee ni wewe ndiye..." "Ni mimi ndiye niliyemuua mpenzi wako Burhan kwa mkono wangu huu." Burhan alimkatisha.

"Muuaji mkubwa wewe, sasa unangoja nini niue basi na mimi." Mwanaidi alianza kulia upya kwa uchungu.

"Nadhani umesahau kwamba ni wewe ndiye uliyeniambia ningoje kwanza, nilipotaka nikufyatulie rirasi ya kichwa." Alimkumbusha.

"Kakukosea nini jamani...kumbe mimi nimekamatwa kila mtu anajua mimi ndiye muuaji, kumbe wewe. Ulimwengu wote haukutaka kuamini kuwa mimi siye niliyemuua Burhan."

"Na utaamini kuwa wewe ndiye muuaji hadi kiama. Kwa sababu mtu wa kwanza kujua kuwa mimi ndiye niliyemuua Burhan ni wewe. Na kwa bahati nzuri utakufa muda si mrefu ujao, hivyo utaondoka na siri hii itaendelea kubaki kwangu tu. Hakuna mtu yoyote duniani, hata hao polisi wako hao hawatojua chochote." Alisema Martin akitabasamu. Tabasamu ambalo Mwanaidi aliliona ni kama linatoka kwa shetani mwenyewe.

"Halafu kwa sababu tu usisumbuke na kesi, na tayari una kesi nyingine, nakufanyia uungwana tu, ni bora nikuue ukapumzike kwa amani."

Mwanaidi anajua kama hajaua. Na hakutarajia kusikia, Martin aliyejitambulisha ni rafiki wa Burhan ndiye muuaji. Lakini alishangazwa na jinsi alivyoingia ndani ya gesti hiyo bila kujulikana na kuondoka.

Akakumbuka pia kuwa hata ule mfuko alioubeba ambao baadaye polisi walimhoji na kudai ulikuwa na pesa zaidi ya milioni 100 ambazo hazikuonekana baada ya kuuawa kwa Burhan. Na ni yeye ndiye anayetajwa kuzichukua.

"Wewe ndiye uliyechukua ule mfuko mwekundu? Na pia utakuwa umeshirikiana na yule kaunta kumuua mpenzi wangu."

**Mwanaidi anajua kama hajaua. Na hakutarajia kusikia, Martin aliyejitambulisha ni rafiki wa Burhan ndiye muuaji. Lakini alishangazwa na jinsi alivyoingia ndani ya gesti hiyo bila kujulikana na kuondoka.**

"Mtamuonea bure yule kaunta wa watu, hajui chochote." Alitabasamu.

"Kwa kukusaidia tu Mwanaidi ni kwamba kifo kile alikitaka mwenyewe mpenzi wako. Nisingemuua kama angemaliza kazi na kuzileta pesa ubaoni kila mtu akachukua mgao wake. Baada ya kuwapa kazi ya kwenda kupora pesa kwa mchongo na mchoro niliolетewa na Tika, huyu mfanyakazi wa benki ambaye umemuua leo kwa sumu, nilimwambia azilete saiti. Yeye akataka kunizidi akili. Walipozipora na wenzake watatu, badala ya kuzileta, yeye akawaua wenzake kwa lengo la kutoroka na pesa zote. Maiti akazitupa Kimara. Nadhani ndiyo akaja kwako. Lengo ikiwa akitoka pale gesti akimbie na pesa zote. Hakujua kuwa mimi kazi hizi za ujambazi nilizianza tangu nina miaka 18. Wakati wanapora mpaka anafanya mambo yake, mimi nilikuwa nawafuatilia bila kujua na gari yangu. Na mwisho wa siku nikamuona ameingia na mwanamke kwenye gesti ya Tukutane Kigogo, ambaye ni wewe. Ndiyo nikafanya ile bila kuacha alama yoyote wala ushahidi na kila kiumbe duniani kikajua kuwa wewe ndiye muuaji." Akasita na kuachia tabasamu kana kwamba alikuwa amefanya jambo la kishujaa.

"Labda unajiuliza, niliingiaje mle ndani na nilimuuaje? Nitakueleza kila kitu, kwa sababu leo hii mmoja atakuwa marehemu na mwingine atabaki duniani akiishi kwa raha. Ni mchezo mdogo sana."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

HABARI MICHEZO



# MBAPPE AONGOZA KWA THAMANI DUNIANI

**PARIS,** Ufaransa


NYOTA wa Klabu ya Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe, ndiye mchezaji mwenye thamani kubwa zaidi duniani kwa sasa, kwa mujibu wa Kampuni ya KPMG's Football Benchmark.

Mbappe mwenye umri wa miaka 22, yupo kwenye kiwango bora kabisa kinachompeleka kuwa mchezaji bora zaidi duniani akiwa pale PSG.

Mbappe hivi karibuni aliwafunga Barcelona mabao matatu 'hat-trick' wakati akiisaidia PSG kushinda 4-1 kwenye mchezo wao kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 bora pale katika dimba la Nou Camp.

Kampuni ya utafiti wa thamani za wachezaji ya KPMG's Football Benchmark, imebainisha kwamba, Mbappe ambaye tayari ameshashinda ubingwa wa Kombe la Dunia akiwa na kikosi cha Ufaransa mwaka 2018, ndiye mwanasoka wa thamani ya juu zaidi duniani kwa sasa.

Thamani yake inatajwa kuwa ni pauni milioni 159, licha ya mtikisiko wa kiuchumi unaosababishwa na janga la virusi vya corona.



## *Pogba bado kurejea dimbani*

**MANCHESTER,** England

PAUL Pogba anatarajiwa kuendelea kuwa nje ya uwanja kwa muda wa wiki moja zaidi pale Manchester United, kwani bado anauguza majeraha yake.

Wakati Man United ikilazimisha sare ya bila kufungana na Real Sociedad kwenye mchezo wa Ligi ya Europa juzi, Alhamisi na kusonga mbele hatua inayofuata, yeye hakuwa sehemu ya kikosi kilichoanza.

Pogba alipata maumivu kwenye mchezo dhidi ya Everton wa Ligi Kuu England ambao ulimalizika kwa sare ya kufungana mabao 3-3, Februari 6 baada ya kupata maumivu ya nyama za paja.

Tayari amekosekana kwenye mechi tatu katika mashindano yote chini ya kocha, Ole Gunnar Solskjaer ambaye anapambana kumsaka mbadala wa Mfaransa huyo.

Solskjaer amesema: "Paul bado hajawa fiti na atakuwa nje kwa wiki kadhaa mpaka pale atakapokuwa imara."

## Lukaku atoa ya moyoni Manchester United

**MILAN,** Italia

ROMELU Lukaku amenukuliwa akitoa ya moyoni kuhusu mwenendo wa klabu yake ya zamani ya Manchester United chini ya kocha Ole Gunnar Solskjaer msimu huu.

Man United wanashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu England nyuma ya vinara na majirani zao Manchester City. Tofauti ya pointi 10 na mabao 14, zinaitofautisha United na City kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Licha ya kuuzwa na United Agosti mwaka 2019 kwenda Inter Milan ya Italia, Lukaku amekuwa akiifuatilia kwa karibu timu hiyo na amenukuliwa akimzungumzia kocha Solksjaer pamoja na mshambuliaji mwenzake, Marcus Rashford.

"(Solskjaer) anafanya vizuri. Mnapaswa kujua kuwa ninampenda kama kocha na kama binadamu mwingine. Ninamtakia kila la heri," alisema Romelu akinukuliwana Sky Sport Italia kuhusu Solskjaer.

"(Rashford) anakuwa bora kila muda! Ninapenda kumuona akicheza. Kiukweli ni moja ya wachezaji wenye kipaji kikubwa ambao nimewahi kucheza nao."

Lukaku tangu kutua kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A, akiwa na Inter Milan, amekuwa kwenye kiwango bora na cha kuvutia zaidi.



# Mourinho sasa akunwa na Delle

**LONDON,** England

KOCHA wa Tottenham Hotspur amesifia kiwango cha kiungo wake, Delle Alli, baada ya kufunga bao la kichwa, wakati Tottenham ilipoicharaza Wolfsberger 4-0 katika michuano ya Ligi ya Europa.

Ulikuwa msimu mgumu kwa Delle na alikuwa kwenye harakati za kuuzwa na Mourinho, lakini alifurahia usiku huo wa Jumatano kwenye michuano hiyo ya Ulaya baada ya kushindwa kuondoka katika dirisha la Januari.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Mourinho alielezea kiwango kizuri kilichoonyeshwa na mchezaji huyo ambaye alifunga bao moja na kutoa pasi ya mwisho moja.

Alli alifunga bao maalumu la ufunguzi dakika ya 10 kisha akawatengenezea pasi za mwisho, Carlos Vinicius ambaye alifunga la pili na bao alilofunga Gareth Bale.

"Sitaki kuzungumzia bao alilofunga, kwa sababu kila mtu ameliona na ninaamini duniani kote walikuwa wakifuatilia mchezo huu, na watu watalitizama hakuna uhitaji wa kuliongelea," Mourinho alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Lakini kwa upande wangu mimi kiwango cha kimataifa alichoonyesha ndiyo muhimu. Alicheza vema sana kwa kila kitu katika mchezo, alicheza vizuri sana."





# DYBALA AFUATA MATIBABU BARCA

**ROME,** Italia

NYOTA wa Juventus, Paul Dybala, ameripotiwa kusafiri kwenda jijini Barcelona nchini Hispania kwa ajili ya kuonana na mtaalamu wa matibabu ya goti, Ramon Cugat.

Nyota huyo ameamua kufunga safari yake kwa ajili ya kwenda kujadili suala la jeraha lake la goti ambalo limekuwa likimsumbua na kuathiri ushiriki wake kwenye mechi.

Dybala mwenye umri wa miaka 27, ameshindwa kuhusika na michezo mingi ya kuanzia Januari, kwa sababu ya jeraha hilo, na alihitaji zaidi kufanyiwa matibabu ya uhakika, na kwa mujibu wa Goal.com.

Mkurugenzi wa Juventus amethibitisha pia kuwa suala la hatima ya nyota huyo klabuni hapo lina walakini kidogo kutokana na kusuasua kwa mazungumzo ya mkataba mpya.

Dybala amesalia na takriban miezi 18 kwenye mkatana wake wa sasa na klabu za Liverpool, Manchester United na Tottenham Hotspur zinatajwa kuwa zinavutiwa na huduma yake na zinalenga kuinasa saini yake.

# *Costa ataka kurudi Juve*

**MUNICH,** Ujerumani

BAADA ya kutolewa kwa mkopo na klabu ya Juventus na kurudi tena Bayern Munich, bado Douglas Costa anataabika kupata namba kwenye kikosi cha miamba hiyo ya soka la Ulaya.

Costa alihusishwa na Manchester United kama mbadala wa Jadon Sancho, lakini mwisho wa siku Juventus waliamua kumtoa Mbrazil huyo kwa mkopo na akarudi tena Bayern.

Kutokana na kukosa namba kwenye kikosi cha kocha, Hans Flick, mchezaji huyo amegusia uwezekano wake wa kurejea Italia.

Kwake anaona ni bora kurudi nchini Italia katika Klabu yake ya Juventus kuliko kuendelea kusugua benchi pale Bayern Munich.

"Nitapenda kurejea Italia, nchi ninayoiheshimu sana. Ngoja tuone kitakachotokea," alisema Coasta akinukuliwa na gazeti la Bild.

"Bado nina mkataba na Juve, hivyo mwisho wa msimu nitarudi kule na naamini nitapambana na kurudisha nafasi yangu.

"Maisha hapa Beyern Munich yamekuwa magumu kwangu, hivyo njia rahisi ni kurudi kwenye timu niliyoizoea na naamini nitapata nafasi ya kucheza."

Coasta alikuwa na kiwango cha kuvutia zaidi katika misimu miwili mfululizo wakati akicheza kule Juventus, lakini ghafla akajikuta kwenye wakati mgumu wa kupambania namba kabla ya kutolewa kwa mkopo.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA: WILLIAN CHACHU YA USHINDI WA ARSENAL

●●● Nafikiri alibadilisha mchezo, alicheza kwa kujituma na alitengeneza ubunifu mzuri...

**ANTHENS,** Ugiriki

MIKEL Arteta amemtaja Willian kwa "kubadilisha mchezo" dhidi ya Benfica wakati Arsenal waliposonga mbele kutoka hatua ya timu 32 kwenye Ligi ya Europa juzi, Alhamisi.

**Arsenal, walionekana kuwa bora zaidi kwenye mchezo huo wa pili baada ya ule wa kwanza kutoka sare na sasa wamefuzu hatua ya mtoano baada ya ushindi huo, kwenye mchezo uliopigwa katika ardhi ya Uingereza.**

Bao la Diogo Goncalves na lile la Rafa Silva yalifuta lile la uongozi la Pierre-Emerick Aubameyang na kuwafanya Benfica kuongoza kwa jumla ya mabao 3-2 kufuatia sare ya bao 1-1 kwenye mechi ya awali.

Thomas Partey na Willian waliingizwa dakika mbili baadaye na wawili hao wakabadili kabisa mchezo wa Arsenal.

Aubameyang alifunga bao la ushindi kwa kichwa zikiwa zimesalia dakika tatu mpira kumalizika na kuifanya Arsenal kusonga mbele kwa uwiano wa mabao 4-3.

"Willian, nafikiri alibadilisha mchezo," alisema Arteta akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo. "Alicheza kwa kujituma na alitengeneza ubunifu mzuri, alitengeneza muunganiko mzuri sana."

Willian katika mchezo huo, alikamilisha asilimia 94 ya pasi zake 17 - ikiwa ni bora zaidi kuliko mchezaji yeyote wa Arsenal kwenye mchezo huo.

"Kwa uhakika kabisa timu ilikuwa kwenye kiwango kizuri na wachezaji walionyesha njaa ya kutaka kushinda na hilo ndilo linalotakiwa katika kila mchezo.

"Tulistahili kushinda na tulishinda. Ingawa mchezo ulikuwa mgumu kwetu, lakini tulipambana kwa kadri tulivyoweza kushinda mchezo ule.

"Tulionyesha mfano mzuri wa majaliwa mazuri ya baadaye kwa mechi zinazofuata."

Aubameyang sasa amefikisha mabao 13 aliyofunga kwenye mashindano yote msimu huu.

## ZISIKUPITE

### MBAPPE AKARIBIA KUSAINI

MGURUGENZI wa Michezo wa Paris St-Germain, Leonardo, amesema muda umekaribia wa kufanya maamuzi wakati klabu hiyo ikitarajia kumshawishi mshambuliaji wake, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 22 kusaini mkataba mpya. ***(France Bleu)***

### SARRI AKUBALI KURUDI CHELSEA

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Maurizio Sarri, alikubali kurudi Stamford Bridge Januari kabla ya 'Blues' hao kumleta Thomas Tuchel kama mrithi wa Frank Lampard aliyetimuliwa. (***RAI Sport, via Star)***

### CITY WAJITOSA KWA HAALAND

KLABU ya Manchester City inapanga kuwa mshindani wa Chelsea katika mbio za kuwania kumsajili straika wa Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20, kutoka Borussia Dortmund kipindi cha majira ya joto. ***(Star)***

### PSG WAMTAKA WIJNALDUM

PARIS St-Germain na Inter Milan zinawania kumsajili kiungo wa Liverpool na Uholanzi, Georginio Wijnaldum mwenye umri wa miaka 30, kama mchezaji huru kipindi cha majira ya joto. ***(Le Parisien)***

### UNITED KUIPA OFA WEST HAM

MANCHESTER United inapanga kuwapa West Ham United ama kiungo Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 28, Nemanja Matic, 32, au Phil Jones mwenye umri wa miaka 29, ili kubadilishana na Declan Rice mwenye umri wa miaka 22. ***(90min)***

### NEYMAR NA MKATABA MPYA

MAZUNGUMZO ya Klabu ya PSG na mshambuliaji wa Brazil, Neymar mwenye umri wa miaka 29, yapo kwenye "njia sahihi", kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Michezo wa klabu hiyo, Leonardo. ***(Mirror)***

### BURNLEY KUMUUZA POPE

KLABU ya Burnley itataka pauni milioni 50 ili kumuachia golikipa wake, Nick Pope mwenye umri wa miaka 28 raia wa England. ***(Lancs Live)***

### EDOUARD KUONDOKA CELTIC

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Odsonne Edouard mwenye umri wa miaka 23, anapanga kuondoka Celtic na amekuwa akihusishwa na klabu kadhaa za Ligi Kuu England, ikiwamo Aston Villa. ***(Birmingham Live)***

### SATRIANO NA ARSENAL, CHELSEA

STRAIKA wa Inter Milan, Martin Satriano mwenye umri wa miaka 20 raia wa Uruguay, anahusishwa na kuwaniwa Arsenal na Chelsea na yeye mwenyewe anataka kuhamia Ligi Kuu England siku moja. ***(Mail)***

### TZOLIS KUUZWA MAN UNITED

KLABU ya Ugiriki ya PAOK inaweza kuwauzia Manchester United, Christos Tzolis wanayemhitaji kwa pauni milioni 17. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19 raia wa Ugiriki anawaniwa pia na Barcelona na Borussia Dortmund. ***(Sun)***

## HABARI MICHEZO

# Kocha Polisi asikitika kupigwa wiki Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa timu ya Polisi, Yusuph Sape, amesema bado ataendelea kukumbuka kipigo cha mabao 7-0 (wiki) dhidi ya Mafunzo katika mchezo wa Ligi Kuu Zanzibar.

Sape aliyasema hayo wakati akizungumza na gazeti hili baada ya kumalizika mchezo huo uliopigwa katika uwanja wa Mau A juzi.

Alisema kipigo hicho kwake yeye kama kocha ni cha kwanza kumkuta tangu aanze kuifanya kazi hiyo kwenye Ligi Kuu Zanzibar.

Alisema katika michezo ya Ligi Kuu, timu kufungwa mabao mengi ni kitu ambacho hakileti taswira nzuri mbele ya mashabiki wa timu hiyo.

"Timu ya Ligi Kuu kufungwa mabao saba ni mengi mno, hii itachukua muda hata mashabiki kuamini timu yao tena, ila mimi naomba wasivunjike moyo," alisema.

Aidha, alisema kilichochangia kufungwa idadi hiyo ni kutokana na karibu nusu ya kikosi chake cha kwanza kuandamwa na majeraha ambayo yatawafanya kuchukua muda kabla ya kurejea uwanjani.

# Tenisi wajipanga kulinda heshima

**Na Shufaa Lyimo**

WACHEZAJI wa tenisi wa hapa nchini wameahidi kufanya vizuri katika mashindano ya Afrika Mashariki na Kati yatakayofanyika leo, Jumapili kwenye Uwanja wa Gymkhana Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili juzi, Kocha wa timu ya Klabu ya Gymkhana, Salum Mvita, alisema mashindano hayo yatahusisha wachezaji wakubwa na nyota wake wamejiandaa vema.

Mvita alisema nchi zote za Afrika Mashariki (Kenya, Uganda na wenyeji Tanzania), pamoja na Zambia zimethibitisha kushiriki mashindano hayo ya mwaka huu.

"Maandalizi kuelekea kwenye mashindano hayo yanaendelea vizuri na wachezaji wapo tayari kwa mashindano hayo ambayo yatakuwa na ushindani mkubwa," alisema Mvita.

Kocha huyo amewataka wadau wa mchezo huo kujitokeza kwa wingi kuwashangilia wachezaji wao ambao kila mmoja ameweka malengo ya kuchukua medali katika michuano hiyo.

"Tunawakaribisha mashabiki wetu kuja kushuhudia vipaji, klabu yetu imejipanga na kila mmoja ana nia ya kuipa ushindi nchi yake, njooni muone vipaji vitakavyokuwa vinaonyeshwa na wachezaji wetu," Mvita alisisitiza.

# TALIB AKUNWA KIWANGO CAF SIMBA, AITABIRIA MAKUBWA

**Na Saada Akida**

ALIYEKUWA mchezaji na Kocha wa Simba, Talib Hilal, amesema anaamini kwa uwezo wa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mfaransa Didier Gomes, hakutakuwapo na vichapo vya mabao 5-0 timu hiyo itakapokuwa ikicheza ugenini katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

> **Msimu wa 2018/19 katika michuano hiyo hatua ya makundi, Simba ikiwa chini ya kocha Mbelgiji Patrick Aussems, ilikubali kipigo cha mabao 5-0 ilipokuwa ugenini Misri dhidi ya Al Ahly na DR Congo dhidi ya AS Vita.**

Hata hivyo, katika hatua ya makundi ya michuano hiyo msimu huu, Simba imeanza kwa kushinda 1-0 ugenini dhidi ya AS Vita, huku ikiendeleza ushindi wa bao 1-0 nyumbani dhidi ya Al Ahly kama ambavyo iliifunga msimu wa 2018/19 ziliporudiana hapa nchini katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Hilal alisema tatizo la kufungwa mabao mengi siku za nyuma sasa limekwisha Simba ikiwa chini ya Gomes, ambaye ameonyesha anajua kutengeneza muunganiko mzuri wa timu uwanjani kwa wachezaji wote kucheza wakisaidia safu ya ulinzi.

Alisema mwanzo Simba walikuwa wanacheza huku mabeki wakifunguka, tofauti na kocha Gomes ambaye amekuja na mbinu nyingi zinazosaidia kuimarisha safu ya ulinzi hususan mabeki wa kati.

"Nategemea kwa mchezo waliocheza juzi, Simba wataweza kufika mbali, ukiangalia utulivu na nidhamu, lakini uwezo wa Joash Onyango na Taddeo Langwa kwa kweli wameongeza nguvu kwenye timu.

"Tuna timu nzuri kikosi kipana, Luis Miquissone, kila mechi anapanda kiwango, amekuwa msaada mkubwa kwa Simba," alisema Talib.

Alisema kwa upande wake bado hajaridhishwa na kiwango cha Clatous Chama anavyocheza, kwa kuwa hajajitoa hata kwa asilimia 50 ya kiwango chake kwenye mechi za msimu huu, hivyo anategemea kuona makubwa zaidi kwa nyota huyo endapo atajirekebisha na kurudi ubora wake.

Alisema kwa mchezo aliouona dhidi ya Al Ahly anaamini Simba itafanya vizuri kwa kuwa inacheza kwa nidhamu ya hali ya juu na kiufundi huku wakiwanyima nafasi wapinzani wao kucheza mpira waliouzoea.



Mchezaji wa KMC, Keneth Masumbuko, akimtambuka (akimruka) mchezaji wa timu ya Kurugenzi ya Simiyu, katika mchezo wa Kombe la FA, uliopigwa Uwanja wa Uhuru Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Msimu Tuzo za WIMA wazinduliwa rasmi*

**Na Mwandishi Wetu**

MSIMU wa pili wa tuzo za kuwapongeza wanawake viongozi barani Afrika zijulikanazo kama "WIMA Awards" umezinduliwa rasmi Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa tuzo hizo juzi, Mkurugenzi Mkuu wa CV People of Tanzania, Naike Moshi alisema, Tuzo hizo za WIMA zitatolewa Machi 27, mwaka huu.

"Tunajivunia kuwa sehemu ya hadithi ya mafanikio ya wanawake viongozi mbalimbali hususan hapa nyumbani na nje ya Tanzania kupitia tuzo hizi za WIMA.

"Kwa mwaka huu tumeongeza vipengele vingine saba vya ushiriki ikiwamo SDG Female Champion, WIMA Stem Awards, Next Gem WIMA Awards, "He for She" Leadership Awards, WIMA Abilities Award, WIMA Lifetime Award na Exemplary Female Leadership During Covid-19 Crisis," alisema.

Alisema tuzo hizo ni za wazi na kila kipengele kitakuwa na washiriki watakaochaguliwa na kupigiwa kura na hatimaye mshindi kupatikana.

"Nina imani kubwa kuwa tuzo za WIMA zitabaki kuwa tuzo kubwa zaidi barani Afrika katika kuwahamasisha na kuwatambua wanawake wanaofanya vizuri katika nafasi mbalimbali za uongozi," alisema Naike.

Kwa upande wa mwakilishi kutoka UN Global Compact Network Tanzania, Marsha Yambi, alisema wanafurahia kuwa sehemu ya tuzo hizo na ni wazi kuwa zimefungua milango mingi kwa wanawake na mashirika mbalimbali kupata nguvukazi inayoleta matokeo chanya kwa uchumi wa nchi.

"Hivyo sisi, UN Global Compact tumeona kuwa tuna jukumu kubwa kuhakikisha kuwa tunashirikiana na taasisi mbalimbali zilizopo nje na ndani ya Tanzania kama CV of People of Tanzania kuhakikisha kuwa tunaleta mapinduzi chanya katika kuboresha usawa wa kijinsia hususan katika maeneo ya kazi.

"Kwa taarifa zaidi kuhusiana na tuzo tembelea tovuti yetu info@wima.co.tz kurasa zetu za kijamii @womeninmanagementafrica LinkeIn na Instagram," alisema Marsha.

# Michezo

Jumamosi Februari 27, 2021

Nipashe




Arteta: Willian chachu ya ushindi wa Arsenal UKURASA 22

## TUMETISHA...



Straika Pierre-Emerick Aubameyang (kushoto) akipongezana na Bukayo Saka aliyemtengenezea mabao mawili dakika ya 21 na 87 wakati Arsenal ikishinda 3-2 dhidi ya Benfica na kufuzu hatua ya 16-bora ya Ligi ya Europa kwenye mchezo uliopigwa Uwanja wa Emirates juzi. Bao lingine la Arsenal lilifungwa na Kieran Tierney dakika ya 67, wakati ya Benfica yakifungwa na Diogo Gonçalves na Rafa. **PICHA: MTANDAO**

## Simba, Namungo zaweka historia

**Na Adam Fungamwango**

HISTORIA imeandikwa nchini kwa timu mbili za Tanzania kutinga hatua za makundi ya makombe makubwa barani Afrika kwa wakati mmoja, baada ya juzi Namungo FC kufanikiwa kufuzu hatua hiyo kwenye Kombe la Shirikisho barani Afrika, CAF.

Namungo, pamoja na kuchapwa mabao 3-1 na timu ya Clube Desportivo Primeiro de Agosto ya Angola, imefuzu kwa jumla ya mabao 7-5 kutokana na kushinda mabao 6-2 kwenye mchezo wa awali. Michezo yote ilichezwa nchini Tanzania kwenye Uwanja wa Azam Complex, wa kwanza ukihesabika kuwa ni wa ugenini, baada ya timu hiyo kuzuiliwa kuingia nchini Angola kwa kile walichodai ni kuzuia kuenea maambukizi ya virusi vya corona.

Namungo inaungana na Simba ambao tayari ilikuwa imeshatinga hatua ya makundi na tayari imeshacheza mechi mbili dhidi ya AS Vita ya Congo DR na Al Ahly ya Misri na zote kushinda kwa bao 1-0.

Hii ni mara ya kwanza kwenye historia ya soka la Tanzania kwa timu zake zote mbili kuweza kuingia hatua ya makundi ya makombe hayo makubwa Afrika, Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho kwa wakati mmoja.

Wakati Simba inaiwakilisha nchi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, ikiwa kwenye Kundi A na timu za AS Vita, Al Ahly na El Merreikh ya Sudan, Namungo yenyewe ipo Kundi D, ikiwa na timu za Nkana FC ya Zambia, Pyramids ya Misri, na Raja Casablanca ya Morocco.

# Kim ataja umuhimu wa Yondani Stars

**Na Saada Akida**

## ●●● Samatta, Msuva kuikosa Kenya na nyota wote wa Simba akiwamo Manula na Mkude ambaye...

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Kim Poulsen, ametangaza kikosi cha timu hiyo kitakachojiwinda na mechi mbili za kirafiki za kimataifa dhidi ya Kenya kujiandaa na mechi za kuwania kufuzu AFCON, huku akimrejesha kikosini beki wa zamani wa Yanga kwa sasa Polisi Tanzania, Kelvin Yondani.

**Tangu ashindwane na Yanga katika makubaliano ya mkataba mpya kwenye usajili wa dirisha kubwa, Yondani aliyejiunga na Polisi Tanzania katika dirisha dogo, Januari mwaka huu, hajaitwa tena kwenye kikosi cha Taifa Stars kilichokuwa kikinolewa na Mrundi Etienne Ndayiragije, lakini jana kocha mpya wa Stars, Poulsen alitangaza kikosi chake na kumjumuisha mkongwe huyo huku akitoa sababu ya kumrejesha.**

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Poulsen alisema kigezo kikubwa cha mchezaji kuwapo timu ya taifa ni kujitoa na kucheza kwa moyo na mpira wa kisasa unahitaji kujitoa sana, hivyo anahitaji wachezaji wanaotaka kujifunza, kukua na kufanikiwa kwa pamoja kama timu.

"Nimewaangalia kupitia mechi zinazorushwa 'live' (mubashara), lakini nimeongea na makocha wa timu zao za ligi ili kupata taarifa za utimamu wa afya kwa wachezaji husika.

"Pia nimechagua wachezaji wengi kwa sasa ili kupata nafasi ya kuwaona zaidi na tutakuwa na kambi hapa Dar es Salaam ya siku kama sita, lakini hatutakuwa na wachezaji wa nje na wale wa timu zinazoshiriki mashindano ya kimataifa, ikiwamo wale wa Simba," alisema Poulsen.

Alisema baada ya siku sita wataenda Nairobi kuweka kambi na kucheza michezo miwili ya kirafiki dhidi ya Kenya, mchezo wa kwanza ukiwa Machi 15, ambao hawatawahusisha nyota wa Simba na kutoka nje.

"Wachezaji wa Simba watajiunga baada ya kumaliza majukumu ya Ligi ya Mabingwa na tunatarajia watakuwapo katika mechi ya pili Machi 18, nimechagua wachezaji vijana kutoka kikosi cha U-20 na watakaofanya vizuri katika mazoezi bila kujali umri na klabu wanayotoka nitawajumuisha," alisema Poulsen.

Kikosi cha Taifa Stars kilichoitwa jana kwa ajili ya mechi hizo mbili za kirafiki kujiandaa na michezo miwili ya kuwania kufuzu AFCON dhidi ya Equatoria Guinea na Libya ni makipa Aishi Manula (Simba), Metacha Mnata (Yanga) na Juma Kaseja (KMC FC).

Mabeki ni Shomari Kapombe, Mohammed Hussein, Erasto Nyoni, Kennedy Juma (Simba), Hassan Kessy (Mtibwa Sugar), Israel Mwenda, Kelvin Yondani, David Bryson (KMC FC), Bakari Mwamnyeto, Dickson Job (Yanga), Carlos Protus (Namungo), Laurent Alfred (Azam FC), Nikcson Kibabage (Youssoufia FC- Morocco) na Edward Manyama (Ruvu Shooting).

Viungo: Simon Msuva (Wydad AC-Morocco), Hassan Dilunga, Jonas Mkude, Mzamiru Yassin, Said Ndemla (Simba), Ayoub Lyanga, Salum Aboubakar Sure Boy, Iddi Selema Nado (Azam FC), Novatus Dismas (Macab Tel Aviv-Israel), Fei Toto, Farid Mussa (Yanga), Himid Mao (El Entag SC- Misri), Ally Msengi (Stellenbosch- Afrika Kusini) na Baraka Majogoro (Mtibwa Sugar).

Washambuliaji: Ditram Nchimbi (Yanga), Mbwana Samatta (Fenerbahce -Uturuki), Thomas Ulimwengu (TP Mazembe - DR Congo), John Bocco (Simba), Yohana Nkomola (Inhulets Petrove- Ukraine), Shaaban Chilunda (Moghreb FC- Morocco), Deus Kaseke (Yanga), Abdul Hamis Suleiman (Coastal Union), Kelvin John (Brooke House College-Uingereza), Nassor Saadun Hamoud (MFK-Czech) na Meshack Abraham (Gwambina).

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >